

**Feza** kuwa karibu na D'Baji

UKURASA 20



**Tottenham** sasa kumbakiza Bale

UKURASA 21

**MAISHA**

MEI 16, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Wazazi wasitafute mchawi mtoto kibaka**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Pendezesha nyumba yako kwa bustani ya mboga



**HARUSI**

Ukurasa 12


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Mei 16, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580582

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




KIPUPWE

**Utakavyojiepusha kukauka ngozi, midomo**

Ukurasa 14

UKURASA 9

# RUNGU LA SAMIA

• **Ma-RC** wawili tu wabakizwa, mabadiliko yatua JKT, TAKUKURU, mabasi ya mwendokasi...*Endelea ukurasa 2*





David Kafulila - **Arusha**



Makongoro Nyerere - **Manyara**



Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge- **Ruvuma**



Rosemary Senyamule- **Geita**



Queen Sendiga - **Iringa**



Meja Jenerali Charles Mbuge - **Kagera**



Stephen Kagaigai- **Kilimanjaro**



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi



Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, CP Salum Hamduni



Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Sylivester Mwakitalu

## NEC yaita mawakala uchaguzi Kigoma

UKURASA 3



## Mzee Mwinyi alivyowakabili 'dadapoa' wa Ulaya

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** KAKOLANYA, GADIEL KUANGUKA 2 UK.23

MAONI, KATUNI UK.6

## Mwinyi alivyowakabili 'dadapoa' wa Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amebainisha alivyokabiliana na wanawake wanaojiuza akiwa masomoni barani Ulaya.

Katika kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mwinyi anaanika kukumbana na mkasa huo wakati akirejea nchini Tanzania kutoka masomoni Uingereza.

Anasimulia kuwa mkasa huo ulimkumba akiwa na wanafunzi wenzake wawili kutoka Zanzibar, ambao ni Dk. Awadhi aliyesomea utabibu na Makame aliyechukua masomo ya utawala.

Mwinyi abainisha kuwa baada ya kuhitimu masomo yao, walipewa hiari ya kuchagua usafiri wa ndege au meli na wote walichagua meli ili wafanye utalii, wakipanda meli ya Afrika Kusini iliyoitwa Doneta Castle.

"Kabla ya kufika Bandari ya Mombasa, meli yetu ilitia nanga bandari maarufu ya Genoa, Italia. Tukatoka melini na kuanza kutembea ufukweni. Mara tukajiwa na dada mmoja wa Kiitaliano, akamwendea na kumkumbatia Dk. Awadhi.

"Kisha akamwita mwenziwe, "Maria! Africano!" Huyo Maria akaja na kwa pamoja wakatualika twende nao mahali ambako walituambia wana vyumba tunakoweza kwenda kupumzika na kustarehe nao.

"Tukajua hawa ni makahaba na tukienda nao yanaweza kutukuta makubwa, ikiwamo pengine kuibiwa na hata kuuawa. "Tukaamua kuwapa pesa kidogo waachane nasi. Ikawa ndiyo mwisho wetu kupunga upepo, tukarejea melini," anasimulia.

Mwinyi pia anataja mikasa mingine miwili waliyokumbana nayo wakiwa ndani ya meli hiyo ukiwamo wa kuwekwa chumba cha watu weusi wakiwa na raia wa Somalia aliyeingizwa akiwa amefungwa pingu.

"Tukajua yule mwenzetu atakuwa mhalifu mkubwa. Tukashauriana kwa Kiswahili juu ya mbinu za kusalimika tuwapo na bwana yule.

"Tukakubaliana tujenge urafiki naye. Tukawa tumechangishana fedha kidogo na kumkabidhi kwa ajili ya matumizi yake, ikiwamo kununulia sigara.

"Kweli akawa rafiki na akatusimulia uhalifu alioufanya akiwa Uingereza, ukiwamo wizi, unyang'anyi, kupigana na kubaka. Basi, urafiki wetu naye ukawa ndiyo salama yetu na tuliendelea naye hadi tulipotia nanga kwenye Bandari ya Mombasa, wakaja polisi wakamtia tena pingu na wakaondoka naye," anasema.

DANSI MKE WA KABURU

Mwinyi anautaja mkasa mwingine katika safari yao hiyo kuwa ni wa kutuhumiwa kumsukuma mke wa kaburu, aliyempiga Dk. Awadhi huku akifoka na kumtusi.

Anasema kuwa baadaye kaburu alirejea kwao na kuwaomba radhi na walipopokea, aliondoka na baadaye wakati wa chakula, aliwafuata tena na kuwataka radhi na kuwapa ofa ya kucheza dansi na mkewe kwa zamu hadi watakapochoka.



Mmoja wa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, akifanya uchambuzi wa majadala ya walimu kwa lengo la kubaini wenye sifa za kupandishwa vyeo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: ADILI MHINA**

# Rungu la Samia latua kwa ma-RC

**Na Romana Mallya**

SIKU mbili baada ya kumsimamisha kazi, Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa na taasisi mbalimbali ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilibainisha Rais Samia pia ameteua viongozi wapya katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (DPP) na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART).

Katika taarifa hiyo, Rais Samia amemteua Anthony Mtaka kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye awali alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu huku Juma Homera akiteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya akitoka Katavi alikokuwa Mkuu wa Mkoa.

Rais Samia amemteua Martin Shigella kuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro akitoka Tanga alikokuwa Mkuu wa Mkoa na anachukua nafasi ya Loata Ersto Ole Sanare ambaye amemaliza muda wake.

Robert Luhumbi ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, akitokea Geita alikokuwa na cheo hicho hicho, huku Albert Chalamila akiteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza akitoka kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya.

Zainab Telack ametoka kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kwenda Lindi anakochukua nafasi ya Godfrey Zambi ambaye amestaafu.

Rais Samia amemteua Brigedia Jenerali Marco Gaguti kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara. Kabla ya uteuzi, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera na anachukua nafasi ya Gelasius Byakanwa ambaye atapangiwa majukumu mengine.

Aboubakar Kunenge ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani akitoka kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na anachukua nafasi ya Evarist Ndikilo ambaye amestaafu.

Wengine ni Joseph Mkirikiti ambaye anakwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara na anachukua nafasi ya Joachim Wangabo ambaye amestaafu.

Rais pia amemteua Dk. Binilith Mahenge kuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida akitoka kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na anachukua nafasi ya Dk. Rehema Nchimbi ambaye amestaafu.

Rais Samia amemteua Dk. Philemon Sengati kuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga. Kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora na amemteua John Mongella kuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu ambaye kabla ya uteuzi huo, alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

Wengine ni Ally Hapi ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora akitokea Iringa na Adam Malima anayekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga akitokea Mkoa wa Mara.

### SURA MPYA

Rais Samia amemteua David Kafulila kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ambaye anakwenda kuchukua nafasi ya Idd Kimanta ambaye amestaafu na Amos Makalla ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akichukua nafasi ya Kunenge ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

Vilevile, Rais amemteua Rosemary Senyamule kuwa Mkuu wa Mkoa wa Geita akichukua nafasi ya Robert Luhumbi ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara na Queen Sendiga, mmoja wa wagombea urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, akichukua nafasi ya Ali Hapi, aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa Tabora.

### JKT, BUNGE, TAKUKURU

Rais Samia pia amemteua Brigedia Jenerali Charles Mbuge kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera ambaye amechukua nafasi ya Meja Jenerali Marco Gaguti aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Kabla ya uteuzi huo, Brigedia Jenerali Mbuge alikuwa Mkuu wa JKT.

Pia, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kuchukua nafasi ya Dk. Anna Mghwira ambaye amestaafu.

Wengine walioteuliwa ni Mwanamvua Mrindoko kuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi, akichukua nafasi ya Juma Homera ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na Brigedia Jenerali, Wilbert Ibuge, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma akichukua nafasi ya Christine Mndeme ambaye ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Rais Samia amemteua Omary Mgumba kuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe ambaye anachukua nafasi ya Brigedia Jenerali, Nicodemus Mwangela ambaye amestaafu na Makongoro Nyerere ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara akichukua nafasi ya Mkirikiti ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa.

### WAWILI WABAKI MIKOA YAO

Rais Samia pia amemteua Thobias Andengenye kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma akiendelea na wadhifa huo mkoani humo na amemteua Marwa Rubirya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe akiendelea na wadhifa huo mkoani humo.

### WATEULE WA TAASISI

Mkuu wa Nchi huo pia amefanya uteuzi wa watendaji wakuu wa taasisi saba, akimteua Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Salum Hamduni kuwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU akichukua nafasi ya Brigedia Jenerali John Mbungo ambaye atapangiwa majukumu mengine.

Taarifa hiyo ya Ikulu pia ilibainisha Rais Samia amempandisha cheo ACP Hamduni kuwa Kamishna wa Polisi (CP) na amemteua Neema Mwakalyelye kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU.

Wengine ni Sylvester Mwakitalu ambaye amemteua kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) akichukua nafasi iliyoachwa na Biswalo Mganga ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu na Joseph Pande ameteuliwa kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), akichukua nafasi ya Edson Makallo ambaye atapangiwa majukumu mengine.

Rais Samia pia amemteua Dk. Edwin Mhede kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa UDART, akichukua nafasi ya John Nguya ambaye uteuzi wake umetenguliwa na amemteua Nenelwa Mwihambi kuwa Katibu wa Bunge, akichukua nafasi ya Kagaigai ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Kadhalika, amemteua Balozi Joseph Sokoine kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, akichukua nafasi ya Brigedia Jenerali Ibuge ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma.

Taarifa hiyo ilibainisha uteuzi wa viongozi hao ulianza jana na wataapishwa Jumanne alasiri Ikulu jijini Dar es Salaam.

HABARI KITAIFA

# Watoto wanaouza vyuma chakavu kukamatwa

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

JESHI la Polisi limeagizwa kuwakamata watoto wote wenye umri chini ya miaka 18 ambao wanafanya biashara ya kuuza vyuma chakavu badala ya kwenda shule.

Pia limeagizwa kukamatwa kwa wazazi wa watoto hao ili wafikishwe mahakamani kujibu tuhuma za kuwaruhusu watoto wao kufanya biashara wakati wanajua ni wanafunzi na wanapaswa kuwa shuleni.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alitoa agizo hilo hivi baada ya kuona kuwapo kwa wimbi kubwa la watoto kukatisha masomo na kujikita kufanya biashara ndogo ikiwamo ya vyuma chakavu.

Homera kwa sasa ameteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, baada ya mabadiliko yaliyofanywa jana na Rais Samia Suluhu Hassan ya uteuzi wa wakuu wa mikoa mbalimbali. Akitoa agizo hilo, Homera alisema kwa mujibu wa sheria ni kosa mtoto chini ya umri wa miaka 18 kufanyabiashara kwa kuwa anapaswa kuwa shuleni, lakini katika Manispaa ya Mpanda hali imekuwa ni tofauti kwa kuwa watoto wengi wanakatisha masomo na kufanyabiashara na kuwapelekea wazazi wao fedha wanazopata.

"Laiti kama sheria ingeruhusu ningewatandika viboko watoto hao wote na kisha kuwapeleka mahabusu...lakini ninaliagiza Jeshi la Polisi liwakamate ili sheria ichukue mkondo wake, mimi sipo tayari kuona watoto wanakatisha masomo eti wanakwenda kufanya biashara," alisema.

Alisema kuwa iwapo watoto hao wataonekana mitaani wanafanyabiashara hizo badala ya kukamatwa na polisi atajua kuwa mkuu wa kituo cha polisi (OCD) cha Mpanda mjini kazi hiyo imemshinda na atamtaka ahame atafute kituo cha kazi kingine kitakacho mfaa na si kituo hicho.

Mmoja wa wakazi wa kitongoji cha Kawajense mjini Mpanda, Josephine Joseph, alimshukuru mkuu huyo kwa agizo hilo na kusema kuwa hivi sasa katika Manispaa ya Mpanda kumekuwa na tatizo kubwa la watoto kukatisha masomo na kukimbilia biashara.

# Uchaguzi mdogo Muhambwe, Buhingwe leo

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi imesema vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mdogo wa ubunge katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe, mkoani Kigoma na uchaguzi wa udiwani katika kata tano za Tanzania Bara, vina wajibu wa kuweka mawakala kwenye vituo vya kupigia na kujumlisha kura kwa kuzingatia sheria za uchaguzi wanapotekeleza majukumu yao.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Rufani (mstaafu), Semistocles Kaijage, alisema hayo katika risala ya uchaguzi huo mdogo unaotarajiwa kufanyika leo na kushirikisha kata za Buziku (Halmashauri ya Wilaya ya Chato), Bugarama (Halmashauri ya Wilaya ya Geita), Igunga (Halmashauri ya Wilaya ya Igunga), Ligoma (Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru) na Kata ya Miuta iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

Alivitaka vyama vya siasa, wagombea na wadau wa uchaguzi kuepuka kujihusisha na matukio yenye viashiria vya uvunjifu wa amani kwa kuwa jukumu la kulinda amani ni la kila mwananchi na kutaka wahakikishe wanalinda amani kwenye majimbo na kata zinazofanya uchaguzi huo.

Jaji Kaijage alisema sheria na kanuni za uchaguzi zimeweka mamlaka na taratibu zinazotakiwa kufuatwa iwapo kutakuwapo na malalamiko yoyote wakati wa uchaguzi na kuvitaka vyama vya siasa na wagombea kufuata utaratibu huo ili kuufanya uchaguzi huo kuwa huru na haki.

Aliwataka wapiga kura wote waliojiandikisha katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe mkoani Kigoma na kata tano za Tanzania Bara, kujitokeza kupiga kura ili kuwachagua wabunge na madiwani wanaowataka.

"Upigaji kura utafanyika katika vituo vya kupigia kura vilivyotumika wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka jana. Vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni," alisema.

"Watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale tu ambao wamo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwenye majimbo na kata husika na wana kadi zao za mpiga kura. Hata hivyo, Tume kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 61 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Kifungu cha 62 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, imeruhusu wapiga kura ambao wamepoteza kadi zao au kadi kuharibika kutumia vitambulisho mbadala."

Kadhalika Jaji Kaijage amekumbusha katika vituo vya kupigia kura kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na kinamama wanaonyonyesha watakaokuwa na watoto vituoni na kutakuwa na majalada ya nuktanundu katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kuona ili weweze kupiga kura wenyewe.

Alifafanua kuwa kwa wapiga kura wenye ulemavu wa kuona ambao hawawezi kutumia majalada hayo wanaruhusiwa kwenda vituoni na watu watakaowachagua wenyewe kwa ajili ya kuwasaidia kupiga kura.

Uchaguzi mdogo wa ubunge katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe, mkoani Kigoma na uchaguzi wa udiwani katika kata tano za Tanzania Bara, utahusisha idadi ya wapiga kura 303,965 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na vituo vya kupigia kura vitakavyotumika kupigia kura ni 793.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (kulia), akibadilishana mawazo na Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, walipokutana Kibondo mjini, mkoani Kigoma jana. Vyama hivyo vimesimamisha wagombea ubunge katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe, kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo unaofanyika leo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matatizo ya Afrika yatatuliwe na Waafrika wenyewe - Urusi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Urusi limesema linaunga mkono jitihada zinazofanywa na Umoja wa Afrika katika kutatua vikwazo vinavyolikabili bara hilo, likisisitiza matatizo ya Afrika yanahitaji kutatuliwa na Waafrika wenyewe bila kuingiliwa na mataifa mengine.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Mjumbe Maalum wa Rais wa Shirikisho la Urusi kuhusu masuala ya Afrika na Mashariki ya Kati, Mikhail Bogdanov, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

Bogdanov alipongeza jitihada zinazofanywa na Tanzania na Afrika kwa ujumla katika kutatua matatizo ya kiusalama katika eneo la maziwa makuu.

"Tunaunga mkono jitihada zinazofanywa na Umoja wa Afrika katika kutatua changamoto zinazolikabili Afrika kwa kuwa matatizo ya Afrika yanahitaji kutatuliwa na Waafrika wenyewe," alisema.

Bogdanov pia alipongeza jitihada zinazofanywa na Tanzania na Afrika kwa ujumla katika kutatua matatizo za kiusalama katika eneo la maziwa makuu.

Aliongeza kuwa Urusi ni moja ya nchi zinazoamini kuwa Afrika inaweza kutatua matatizo yake bila ya kuingiliwa kutokana na mazingira yaliyopo na kwamba nchi hiyo ipo tayari kushirikiana na Afrika hususani Tanzania katika kuleta amani na usalama sambamba na kuchochea jitihada za maendeleo ikiwamo biashara na uwekezaji.

Waziri Mulamula alimwomba waziri huyo kuimarisha zaidi uhusiano wa diplomasia ya uchumi hususani katika sekta ya biashara na uwekezaji kutokana na takwimu zilizopo kuonyesha kiwango kidogo cha uhusiano wa kibiashara na uwekezaji.

"Tumejadili masuala la kuimarisha uhusiano wa Tanzania na Urusi hasa katika sekta ya biashara na uwekezaji, ambapo Mheshimiwa Bogdanov ameahidi kulifanyia kazi suala hilo na kuhakikisha tunakuza biashara na uwekezaji," alisema Balozi Mulamula.

Alisema Tanzania iko tayari kuwa mwenyeji wa mkutano wa ushirikiano kati ya Urusi na Afrika ambao umepangwa kufanyika Afrika, Umoja wa Afrika ukiwa na jukumu la kupendekeza nchi moja ambayo itakuwa mwenyeji wa mkutano huo. Alimwomba Naibu Waziri huyo kuhamasisha watalii kutoka Urusi kuja kwa wingi nchini na kwamba Tanzania imechukua tahadhari zote zinazosisitizwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu janga la corona.

# Utata waibuka makao makuu ya halmashauri

Na Dinna Maningo, MUSOMA

KUMEIBUKA sintofahamu kuhusu mahali halali pa kujengwa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, huku baadhi ya wananchi na viongozi wakidai Kata ya Murangi ndiyo ilipendekezwa kuwa makao makuu ya halmashauri hiyo huku wengine wakidai Kata ya Suguti ndiyo ilipendekezwa.

Nipashe inafunga safari hadi Kijiji cha Murangi, Kata ya Murangi wilayani Musoma mkoani Mara, mwendo wa kilomita 56 kutoka mjini Musoma kuzungumza na wananchi wanaodai kuporwa makao makuu na kuhaimshiwa Kata ya Suguti.

Wananchi wanadai baada ya makao makuu kupendekezwa kujengwa Murangi, wananchi waliamua kutoa ardhi yao bure ya hekta 245.82 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za makao makuu ya halamshauri.

Vilevile, wanadai walifanya harambee ya kuchanga fedha zaidi ya Sh. milioni 100 zilizowekwa kwenye akaunti ya Halmashuri ya Musoma kwa ajili ya upimaji na kujenga miundombinu ya barabara ili kurahisisha shughuli za upimaji.

Wilson Lusanyu, mmoja wa wananchi hao, anadai kuwa Januari 17, 2013, aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, John Tupa, alifanya mkutano na wananchi kutaka wamweleze kama wameridhia kutoa maeneo yao na walimhakikishia kutoa maeneo yao bure na kisha alitembelea maeneo yaliyotolewa na wananchi kwa ajili ya kujenga makao makuu.

"Tupa alifanya kikao na wananchi wakamweleza wametoa ardhi yao bure kujenga makao makuu, bahati mbaya alishatangulia mbele za haki Mungu amlaze mahali pema peponi na michakato yote ya vikao ikafanyika, leo tunaambiwa eti makao makuu si Murangi bali ni Suguti.

"Moja ya sifa ya Murangi kuwa makao makuu ni kwa sababu ndiyo kata ambayo ipo katikati na hapa Murangi ndipo Rais wa kwanza Julius Nyerere aliyetangulia mbele za haki, mwaka 1954 alilala hapa Murangi kwenye nyumba ya Daniel Kerenje wakati anakitangaza chama cha TANU na kutafuta wanachama kujiunga na TANU, ikapendekezwa Murangi ijengwe kama kumbukumbu na kuenzi harakati zake," alisema.

Lusanyu (82), anasema kuwa baada ya wananchi kutoa ardhi yao, kulifanyika harambee ya kuchanga fedha mwaka 2014 iliyoongozwa na Mbunge wa Musoma Vijijini wakati huo akiwa Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo, na zaidi ya Sh. milioni 100 zilichangwa na wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Oktoba 6, 2014 wananchi walikabidhi rasmi ardhi yao kwa serikali kujenga makao makuu ya halmashauri, pesa zikatumika kwenye mchakato wa upimaji na kujenga madaraja manne ili kurahisisha miundombinu ya barabara, wananchi wameachia maeneo yao miaka mingi halafu leo unawaambia kuwa hakutajengwa makao makuu, hii inaingia akilini kweli?" anahoji Lusanyu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu

Jeni Mgeta, aliyekuwa miongoni mwa wajumbe wa kamati ya upimaji adhi katika eneo lililotolewa kujengwa makao makuu huko Murangi, anasema anashangazwa na uvumi unaoendela kwamba ardhi iliyolotolewa na wananchi, udongo wake haufai kujengwa ghorofa na serikali haikuwahi kufika kuwaeleza kitaalamu kama udongo huo haufai kujenga nyumba zikiwamo za ghorofa.

"Wanasema wananchi wa Murangi wamekatalia maeneo, hivi kweli tulikatalia maeneo wakati wataalamu wa ardhi na mipango miji wanakuja kupima tukiwa tumeongozana nao? "Mbona wananchi hawakuwafukuza kutoka kwenye maeneo, mbona walifanya upimaji wakamaliza salama na wakaondoka na wamekuwa wakifika mara kadhaa hakuna aliyewahi kuwafukuza?

"Wengine wanasema ardhi ni mbaya, haifai kujenga ghorofa. Kama haifai, mbona hatukuambiwa na wataalamu wa udongo? Mbona kuna ghorofa limejengwa hapa na haijaporomoka?

"Hatua zote za upimaji zilifanyika na wakasema makao makuu yatakuwa Murangi na hata vikao vya Baraza la Madiwani vilikuwa vikifanyika Murangi.

"Kama Murangi haikupendekezwa kuwa makao makuu ya halmashauri, kwa nini baadhi ya vikao vya Baraza la Madiwani vilifanyika hapa Murangi?" anahoji.

Kaimu Mwenyekiti wa Kijiji cha Murangi, Amos Mwigamba, anasema wananchi wa kijiji hicho wamekuwa wakiandika barua za kukazia juu ya kutoa eneo bure kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu.

Anasema iwapo serikali imesitisha, inatakiwa kuwalipa wananchi fidia ya kutotumia ardhi yao ambayo waliikabidhi, pia kurejesha fedha zilizochangwa kwa ajili ya upimaji wa maeneo.

"Machi mwaka huu walikuja wataalamu wa ardhi, wakasema wamekuja kupima, wakapima viwanja 700 vya kuanzia ujenzi wakawaambia wananchi kila mtu asimame kwenye eneo lake, wakasimama wakapigwa picha lakini cha kushangaza siku chache tunaambiwa madiwani wamepitisha makao makuu kujengwa Suguti.

"Kwa hiyo, wananchi waliopigwa picha waliwapiga ili waseme kuwa walikataa kutoa ardhi yao, kwa nini wabadilishe tena? anahoji.

Aliyekuwa Diwani wa Murangi (2005-2010), Steve Magafu, anasema Baraza la Madiwani ndilo lililoanzisha mchakato wa kuomba halmashauri na madiwani walikubaliana Murangi kuwa makao makuu ya halmashauri.

"Tuliomba tuwe na wilaya lakini tukashauriwa tuanze na halmashauri wakati huo tuliomba wilaya iitwe Nyanja na halmashauri iitwe Halmashauri ya Nyanja na Jimbo la Nyanja ili kutofautisha jina la Musoma kwa kuwa kulikuwa na Jimbo la Musoma Mjini, muda wa uongozi ukaisha nikastaafu," anasema.

Magafu anaiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza kiini cha kuhamishwa makao makuu kutoka Murangi kwenda Suguti, akidai kuona mazingira ya rushwa.

Christopher Masamaki, aliyekuwa Diwani wa Murangi 2010-2015, anakiri kulikuwa na mvutano mkubwa wapi pawekwe makao makuu ya halmashauri na baadhi ya madiwani walipendekeza makao makuu yawe Nyambono, wengine Murangi, Tegeruka, Maneke na Suguti lakini hatua ya mwisho iliridhiwa makao makuu kuwa Murangi.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na Diwani Mugango, Charles Nyambita, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri mwaka 2012, anasema kikao cha Baraza la Madiwani kilichoketi Agosti 7, 2012 kilipendekeza makao makuu kujengwa Suguti NA 81 ya kura zilizopigwa zilipendekeza Suguti na asilimia 19 zilipendekeza Murangi, kikao kikihudhuliwa na madiwani 38.

"Kwenye kikao cha chama, madiwani walipendekeza Suguti, DCC walipendekeza Suguti, kikao cha RCC kikakubali Suguti.

"Mwaka 2019 tuliamriwa kuhamia kwenye maeneo ya utawala tukaamua kwenda kata ya Mugango kwa muda na Machi 17, 2021 tumekaa kikao cha kujadili ujenzi wa makao makuu, madiwani wakasema pesa ipo, hawawezi kuvutana, wakapiga kura.

"Kati ya madiwani 28, kura moja ndiyo ilipendekeza Murangi, sisi tumeshaanza ujenzi, wenyewe wazungumze tu, mwenye mamlaka ya kutengua uamuzi wa madiwani ni Rais tu," anafafanua Nyambita.

**KAULI YA TAKUKURU**

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mara, Hassan Mossi, anasema hawajapokea malalamiko yoyote kama kuna viashiria vya rushwa katika mchakato wa makao makuu na kwamba taaisisi hiyo haihusiki na masuala ya michakato ya makao makuu ya halmashauri, bali ni halmashauri na vikao vya Baraza la Madiwani, DCC na RCC.

"Kama kuna watu wanaona kwamba kuna mambo yanafanyika yanayohusiana na vitendo vya utoaji au upokeaji rushwa, watupe ushirikiano na tutafuatilia kufahamu fedha zilizochangwa na wananchi kwa ajili ya upimaji wa viwanja eneo la Murangi, tujue zilichangwa shilingi ngapi, ziliwekwa kwenye akaunti gani na zilivyotumika," anasema Mossi.

**MKURUGENZI ANENA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo, anasema halmashauri ni ya wananchi wanaowakilishwa na madiwani na kwamba yeye hana mamlaka ya kuhamisha makao makuu kutoka Murangi kwenda Suguti, bali ni uamuzi wa baraza la madiwani.

Kuhusu wananchi wa Murangi kuchanga fedha zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya upimaji wa viwanja, mkurugenzi huyo anasema hana taarifa ya fedha kuchangwa na kuahidi kufuatilia.

Anasema suala la makao makuu liliamriwa na baraza la madiwani la 2012 ambapo asilimia 81 walipendekeza makao makuu kuwa Suguti na asilimia 19 walipendekeza Murangi na kwamba hakukuta nyaraka zozote zinazoonyesha makao makuu ni Murangi, bali zilizokuwapo zote zinaonyesha makao makuu ni Suguti.

"Mwaka 2019 wananchi wa Murangi waliombwa kila mtu ambaye ana eneo lake, yeye pamoja na familia yake hata kama ana wajukuu, kila mtu aandike barua kama karidhia kutoa eneo bure lakini hakuna aliyeandika barua na maeneo hayo wanayatumia, wanalima na wamejenga," anasema Kayombo.

"Vikao vilifanyika na Suguti pakapendekezwa kwa kuwa kule kuna eneo la serikali lililokuwa ni la misitu, lilitengwa mwaka 1974 ambalo halina wananchi ambao wangedai fidia, limepimwa lenye hekta 282.6, lina hati tayari, kuna mkandarasi SUMA JKT ndiye atajenga.

**DC MUSOMA**

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Vicent Naano, anasema wananchi wa Murangi walikataa kutoa vielelezo vinavyothibitisha kama wamekubali kutoa ardhi yao bure kujenga makao makuu ya halmashauri na kwamba baraza la madiwani ndilo lenye uamuzi na lilipitisha makao makuu kuwa Suguti.

"Baraza la Madiwani ndilo lenye uamuzi, kikao cha RCC chenyewe kinatoa ushuri tu, unaweza kukubaliwa au ukakataliwa.

"Madiwani wakishapitisha wameridhia, sehemu sahihi ya kujengwa ni sehemu iliyopitishwa na Baraza la Madiwani.

"Kuna vitu vingine siyo vya kuandika, kuna vitu vingine nyie waandishi hamvijui na kuna vingine siyo vya kuandika kwa sababu wewe ni mtu wa migogoro, siwezi kukuambia," anasema.

**WAZIRI WA ARDHI**

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Butiama kabla ya kugawanywa Jimbo la Musoma Vijijini na Butiama aliyeongoza mwaka 2012-2015 na sasa ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Jimbo la Ilemela, Dk. Angelina Mabula, anasema kuwa akiwa mkuu wa wilaya, walikaa vikao na Murangi ilipitishwa kuwa makao makuu na viwanja vilipimwa pamoja na ramani ya makao makuu ya Murangi.

Oktoba 7, 2019, Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli, alitoa agizo la siku 30 kwa halmashauri 31 nchini kuhama mjini na kwenda maeneo ya vijijini katika maeneo ya utawala ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ilitekeleza agizo hilo kwa kuhamia katika makao ya muda Kata ya Mugango ambako ofisi zake ziko kwenye majengo yaliyokuwa kiwanda cha pamba.

HABARI KITAIFA

## Kundi la tembo lazua taharuki mashambani

**Na Said Hamdani,** LINDI

KUNDI kubwa la tembo limevamia kijiji cha Ngumbu, wilayani Liwale na kusababisha uharibifu wa hekari 600 za mashamba ya mazao mchanganyiko na taharuki kwa wananchi wanaotegema kilimo kwa maisha yao.

Taarifa kutoka kijijini hapo na kuthibitishwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa kisiasa na serikali, kundi hilo la tembo limevamia kijiji hicho na kuleta hofu kwa jamii.

Wananchi wanaoishi katika kijiji hicho, Hamza Mparangondo, Juma Hemedi, Asha Kindamba wakizungu mza kwa niaba ya wenzao, wamesema kitendo cha tembo hao kuvamia kijijini hapo kinaleta hofu ya usalama wa maisha yao na kushindwa kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Wamesema kwa kipindi cha wiki moja kundi hilo la tembo limepiga kambi kijijini hapo, huku wakishambulia mazao mashambani mwao, pamoja na wanafunzi kushindwa kwenda shule wakihofia usalama wao.

"Kwa sasa watoto wetu wanaotoka vitongoji vya Amani na Kipenyo wapo majumbani, wakihofia usalama wao," alisema Hamza.

Diwani wa Kata ya Kibutuka, Faraji Mnyihira, alipoulizwa kuhusu uvamizi huo, alikiri kundi kubwa la tembo kuvamia kijijini hapo na kuharibu mazao ya wananchi, yakiwamo mahindi, kunde, mpunga, muhogo, mtama na mikorosho.

Alisema ameshatoa taarifa kwa uongozi ngazi ya wilaya na maofisa wanyama pori ambao wamekwenda kwa ajili ya kuwaondoa bila mafanikio, kwa kuwa bado wanaendelea kuzurura katika maeneo mbalimbali ya kijiji hicho.

Diwani huyo, alisema tayari wananchi wameanza kukumbwa na hofu ya njaa, baada ya zaidi hekari 600 za mashamba ya mazao mchanganyiko kushambuliwa na kuharibiwa na wanyama hao, huku akiomba serikali kuongeza nguvu ya kupeleka askari kijijini hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Sarah Chiwamba, amekiri kundi hilo kuvamia kijiji hicho, na kueleza tayari ameshatuma timu ya askari ya wanyama pori kwenda kusaidiana na waliopo kuwaondoa na kuwarejesha msituni.

"Suala la tembo kuvamia maeneo ya watu ni jambo la kawaida kwani kutokana na wingi wao hata makao makuu ya nchi Dodoma wameonekana," alisema Chiwamba.



Wananchi wakiwa kwenye foleni ya kununua nyama kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitri, eneo la Goba, mkoani Dar es Salaam jana. Kilo moja ya nyama iliuzwa kwa bei ya 8,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Katazo sigara hadharani, kutema mate barabarani

**Na Beatrice Moses**

MARUFUKU ya kutema mate ovyo barabarani, kuvuta sigara hadharani au mahali pa jumuiya au kwenye vyombo vya usafiri, imetangazwa katika Halmashari ya Manspaa ya Ubungo, vinginevyo mhusika atapaswa kulipa faini ya Sh. 200,000.

Hayo ni miongoni mwa mapendekezo yaliyowekwa kwenye mchakato wa kutunga sheria ndogo za halmashauri hiyo, ambapo pia imetoa nafasi kwa wananchi kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo hayo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, katika mkutano wake wiki iliyopita aliwasomea wananchi mapendekezo hayo na kuwataka kufika ofisini kwake ili kutoa maoni yao juu ya rasmi ya sheria ndogo za halmashauri hiyo.

Muro aliwasisitiza wananchi hao kutambua umuhimu wa nafasi yao katika kutoa maoni kwa kuwa sheria hiyo ikipitishwa inapaswa kutekelezwa ipasavyo.

"Sheria zilizokuwa zinatumika, zilichukuliwa kutoka Halmashauri ya Kinondoni, sasa nasi Mtaa wa Saranga tukiwa ndani ya Halmashauri ya Ubungo tushiriki kutoa maoni ili ziletwe sheria ambazo tumemeshiri kuzitoea maoni," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Beatrice Dominic, akizungumza na Nipashe, alisema alitoa maagizo kwa watendaji wa kata kuhusu kuwafikishia rasimu hiyo wananchi na kukusanya maoni yao.

Watendaji hao walitakiwa wahakikishe vikao vya kamati ya maendeleo ya kata (WDC) vinafanyika ndani ya siku 7 kuanzia Mei 3 hadi Mei 9, mwaka huu kisha Mei 10 wawasilishe mihutasari ya WDC kwenye ofisi za halmashauri Kitengo cha Sheria.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, Fotunata Shija, alisema wananchi walipewa siku 14 kuwasilisha maoni yao kupitia kwenye ofisi za serikali za mitaa, waeleze wanavyofikiri juu ya mapendekezo hayo.

"Mchakato bado unaendelea kwenye ngazi ya kata, ambao madiwani watatoa maoni yao nayo pia yatachukuliwa, kisha hatua zitaendelea hadi tutakapoukamilisha na kupata sheria ndogo zitakazotumika rasmi," alisema Shija.

Watendaji wa kata waliagizwa kuhakikisha wanasimamia ukusanyaji wa maoni katika ngazi ya mtaa, pia kuratibu mkutano wa WDC ili kuwezesha wananchi katika makundi mbalimbali kujadili rasimu na kutoa maoni yao.

Mapendekezo mengine yaliyopo kwenye rasimu hiyo ni pamoja na kuzuiwa kufanyika kwa matengenezo ya magari na pikipiki na mitambo kwenye makazi badala yake inatakiwa yafanyike kwenye karakana.

Imependekezwa iwe ni marufuku kuegesha magari kwenye njia ya waendao kwa miguu, mtaa, uchochoro, mtaro na maeneo ya wazi, au kufanya biashara ya kuosha gari, pikipiki na mitambo kwenye eneo la makazi.

Kwenye rasimu hiyo, inapendekezwa iwe marufuku kufuga mifugo ya aina yoyote bia kibali cha halmshauri au kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lisiloruhusiwa.

Marufuku nyingine ni kunganisha maji ya mvua na maji taka au kutapisha choo na kutiririsha vinyesi vya mifugo au binadamu kwenye chanzo cha maji au mfereji wa maji ya mvua.

# Utafiti kubaini watoto wanaoishi mitaani wakamilika

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imekamilisha utafiti wa kubaini idadi ya watoto wanaoishi mitaani na wanakotoka na sasa inaendelea na hatua ya kuwakutanisha na familia zao ili kuondoa wimbi hilo katika miji na majiji.

Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Dk. John Jingu, aliyasema hayo jana wakati wa maadhimisho ya siku ya familia duniani inayobebwa na kaulimbiu; "Familia na teknolojia mpya."

Dk. Jingu alisema kundi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani huchangiwa kwa kiasi kikubwa na migogoro inayotokea kwenye familia na wanafamilia wanapotengana, mtoto hukosa pa kwenda na kulazimika kujilea.

"Wizara tulifanya utafiti katika miji yote na tunajua watoto wapo wangapi mtaani na wanatoka wapi, tumemaliza kuwatambua. Idadi yao ipo, mchakato huu ni endelevu tunaendelea kuwatambua," alisema.

Alisema kwa upande wa Mwanza wameshaanza kuwakutanisha na familia zao ingawa tatizo linalojitokeza wanapokwenda nyumbani wanakutana na migogoro ya familia na kurejea tena mtaani.

"Mwarobaini hapa ni familia, Mwanza tuliwapeleka karibu wote nyumbani, idadi tuliyoitambua ilikuwa ni 900, lakini baada ya siku chache wakarudi wakiulizwa kwa nini, wanasema wamekuta migogoro nyumbani hakukaliki," alisema. Dk. Jingu aliitaka jamii hasa wanandoa isaidie kutunza watoto kwa sababu wanapofarakana madhara huenda kwa watoto ambao hukimbia nyumbani kwenda kufanya kazi majumbani, sokoni na wengine mtaani wakati wanapaswa kuwa shule na elimu ni bure.

Kuhusu teknolojia, alisema licha ya kuwa na faida nyingi, inapotumiwa vibaya huathiri familia na kuzisababishia migogoro na kwa upande wa watoto wamekuwa wakijifunza mambo ambayo hayaendani na maadili ya kitanzania.

"Ni vyema wazazi watambue kuwa wanapowanunulia watoto wao simu za mkononi, kompyuta mpakato lazima kuwe na ufuatiliaji ili kuwaepusha kujiingiza kwenye vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ya Mtanzania, mitandao ya kijamii ikitumiwa vibaya huchangia wakati mwingine watoto kujiunga na makundi mabaya yakiwamo uhalifu wa kimataifa," alisema.

Kuhusu maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa hivi karibuni yanayotaka wadau kusaidia maadili ya vijana, Dk. Jingu alisema wizara imeshaanza kulifanyia kazi na kwamba upo mwongozo ulioandaliwa utakaowasaidia makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini na wa kimila kulishughulikia.

Alisema wizara inaikumbusha familia kuhusu wajibu wa kulinda watoto dhidi ya ukatili ukiwamo wa mtandaoni ambao huleta athari kwa mtoto na baadhi kufikia hatua ya kutaka kujiua.

Pia wizara hiyo imezikumbusha halmashauri na mikoa kuhakikisha wanaendelea na jitihada za kuisaidia jamii kukuza vipato na kutatua migogoro inapotokea.

Kuhusu ukatili dhidi ya wasaidizi wa ndani na shambani, aliwataka wahusika wanapopitia katika hali hizo wasinyamaze kimya badala yake waende kutoa taarifa kwa mjumbe au polisi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila la kheri uchaguzi mdogo Muhambwe, Buhigwe

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi imewakumbusha wapiga kura wote waliojiandikisha katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe mkoani Kigoma na kata tano za Tanzania Bara kujitokeza kupiga kura ili waweze kuwachagua wabunge na madiwani wanaowataka katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika leo.

Pia, vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mdogo wa ubunge katika majimbo hayo, vimetakiwa kuweka mawakala kwenye vituo vya kupigia na kujumlisha kura kwa kuzingatia Sheria za Uchaguzi wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Jaji wa Rufani Semistocles Kaijage, amevitaka vyama vya siasa, wagombea na wadau wa uchaguzi kuepuka kujihusisha na matukio yenye viashiria vya uvunjifu wa amani kwa kuwa jukumu la kulinda amani ni la kila mwananchi na kutaka wahakikishe wanalinda amani iliyopo sasa kwenye majimbo na kata zinazofanya uchaguzi huo. Sheria na Kanuni za Uchaguzi zimeweka mamlaka na taratibu zinazotakiwa kufuatwa iwapo kutakuwapo na malalamiko yoyote wakati wa uchaguzi, hivyo Jaji Kaijage amevitaka vyama vya siasa na wagombea kufuata taratibu hizo ili kuufanya uchaguzi huo ufanyike kwauhuru na haki.

Katika mambo yaliyosisitizwa kuzingatiwa kwenye uchaguzi huo ni wagombea na wafuasi wao kuzingatia kuwa kampeni za uchaguzi zilikamilika jana saa 12:00 jioni na hawaruhusiwi kufanya mikutano ya kampeni kuanzia muda huo na kutumia alama za vyama zinazoashiria kampeni kama vile vipeperushi, bendera na mavazi. Wapiga kura wamekumbushwa vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa 1:00 asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni na iwapo watakuwapo wapiga kura katika mstari ambao walifika kabla ya saa 10:00 jioni na hawajapiga kura, wataruhusiwa kupiga kura, lakini mtu yeyote hataruhusiwa kujiunga katika mstari wa wapiga kura baada ya saa 10:00 jioni.

Vile vile, watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale tu ambao wamo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwenye majimbo na kata husika na wana kadi zao za mpiga kura. Hata hivyo, Tume kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 61 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Kifungu cha 62 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, imeruhusu wapiga kura ambao wamepoteza kadi zao au kadi kuharibika kutumia vitambulisho mbadala.

Mojawapo ya vitambulisho hivyo ni pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kitambulisho cha uraia kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Mpiga kura aliyepoteza kadi au kadi yake kuharibika ataruhusiwa kutumia kitambulisho mbadala iwapo tu atakuwa ameandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na jina lake lipo kwenye orodha ya wapiga kura anapokwenda kupiga kura. Aidha majina yake yaliyopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura yafanane na yale yaliyopo katika kitambulisho mbadala.

Pia, kipaumbele kitatolewa kwa wagonjwa, watu wenye ulemavu, wazee, wajawazito na kinamama wanaonyonyesha watakaokuwa na watoto vituoni na kutakuwa na majalada ya nuktanundu katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kuona ili weweze kupiga kura wenyewe.

Wapiga kura wenye ulemavu wa kuona ambao hawawezi kutumia majalada hayo wanaruhusiwa kwenda vituoni na watu watakaowachagua wenyewe kwa ajili ya kuwasaidia kupiga kura. Kwa kuzingatia maadili ya uchaguzi ya mwaka jana yaliyokubaliwa na wahusika wote vikiwamo vyama vya siasa, wapiga kura watatakiwa kuondoka vituoni baada ya kupiga kura na Tume imewashauri wananchi kujiepusha na mikusanyiko katika maeneo ya vituo vya kupigia kura.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanawake wakae mguu sawa uteuzi

**MOJA** ya mambo ambayo watetezi wa haki za wanawake wanayapigia kelele, ni kuwapo kwa usawa wa kijinsia katika uongozi ili idadi yao katika uongozi ilingane na ya wanaume.

Wanataka hilo lifanyike, kwa kuwa watambua kwamba, uongozi siyo mzigo wa kubeba kichwani au begani bali ni uwezo wa kuongoza na mwanamke hawezi kushindwa kuongoza.

Kutokana na kutambua hilo, baadhi yao wamewahi kuandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake inayohamasisha umuhimu wa kuwateua katika nafasi za uongozi na kuisambaza kwenye ofisi za vyama vya siasa.

Ilani hiyo ilisambazwa kwenye ofisi za vyama vya siasa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana ili viongozi waisome na kuteua wanawake wengi kuwania udiwani na ubunge katika uchaguzi huo.

Walifanya hivyo ili uteuzi uzingatie usawa wa kijinsia na ikiwezekana madiwani na wabunge kati ya wanawake na wanaume, wawe 50 kwa 50 ili kuondoa ubaguzi wa kijinsia katika uongozi.

Nafasi nyingine ambazo wanawake wanazitaka kwa ajili ya usawa wa kijinsia ni pamoja na ukuu wa wilaya, mkoa, ukurugenzi, uwaziri na nyingine za juu zaidi, kwa kuwa wanaamini kwamba uwezo wa kuongoza wanao.

Wanaamini nafasi za uongozi wanazopata, hazijaakisi usawa wa kijinsia na wanaona bado kuna haja ya kuwekwa msukumo zaidi kuhakikisha wanawake wanakuwa wengi kwenye uongozi.

Baada ya kilio hicho cha muda mrefu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ameahidi kuimarisha usawa wa kijinsia kwa kuteua wanawake wengi zaidi katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Rais alitoa ahadi hiyo hivi karibuni wakati akilihutubia Bunge huku akisisitiza kuwa uteuzi huo kuzingatia vigezo na sifa, ambavyo ni pamoja na kuwa na elimu na uwezo wa kuongoza.

Binafsi ninaichukulia ahadi ya Rais ya kutaka kuteua wanawake wengi zaidi katika uongozi kama mwendelezo wa kufuta

> **Nafasi nyingine ambazo wanawake wanazitaka kwa ajili ya usawa wa kijinsia ni pamoja na ukuu wa wilaya, mkoa, ukurugenzi, uwaziri na nyingine za juu zaidi, kwa kuwa wanaamini kwamba uwezo wa kuongoza wanao.**

mfumo dume ambao umekuwapo nchini kwa muda mrefu.

Lakini kwa kuwa kiongozi wa nchi anasisitiza umuhimu wa kuzingatia vigezo na sifa, itapendeza kama wanawake wataelewa msisitizo huo ili pale baadhi yao watakapoachwa, wasilalamike.

Kwa kuwa inaonyesha Rais amedhamiria kuondoa mfumo dume katika nafasi za uongozi ili wanawake wasiendelee kuwa wapigakura tu, kilichobaki ni kumuunga mkono ili lengo lake litimie.

Rais anaonyesha kuwa anataka kuona nchi hii inaongozwa na watu wa jinsia zote kwa uwiano, lakini bado kuna haja ya kuwakumbusha wanawake kuwa kupata nafasi za uongozi ni kwa kuzingatia zaidi vigezo na sifa.

Uamuzi wake huo unaweza kufufua upya matumaini ya wanawake ili kupigania haki na usawa wa kijinsia katika uongozi, hatimaye kuondoa unyanyaji, kudharauliwa na kufanyiwa ukatili.

Ikumbukwe kuwa usawa wa kijinsia katika uongozi, bado ni safari ndefu, kwa kuwa hata katika uchaguzi uliopita, nafasi nyingi za udiwani na ubunge zilichukuliwa na wanaume.

Lakini pamoja na hayo, Tanzania kuwa na Rais mwanamke inaweza kuwa hatua mojawapo kuelekea katika kuzika mfumo dume, hivyo ninaamini iwapo wanawake wote wataungana itakuwa ni rahisi kufuta mfumo dume uliopo.

Njia mojawapo ya kuungana ni pale mwanamke anapojitokeza kuwania uongozi, kuanzia serikali ya mtaa, udiwani au ubunge, wenzake wamuunge mkono kwa kumpigia kura.

Wakifanya hivyo, inakuwa ni rahisi kupata ushindi wa kishindo, kwa kuwa imekuwa ikielezwa kwamba wanawake ni jeshi kubwa ambalo linaweza kuungana na kufanikisha jambo lolote.

Kumekuwapo na dhana kwamba wanawake hawapendani na hawasaidiani pale mmoja wao anapowania uongozi, kwa kuwa wanajiita jeshi kubwa, basi sasa ni wakati wa kuungana ili kuzima mfumo wanaoukataa.

SAFU

AFYA

# Hizi ni faida za kunywa maji ya limao

Na Mwandishi Wetu







MAJI ni afya, uhai, tiba na kinga ya magonjwa mbalimbali.

Unywaji wa maji kwa wingi hasa wakati wa asubuhi una faida nyingi za kiafya.

Tabia ya kunywa maji ya vuguvugu yaliyochanganywa na ndimu au limao humpatia mtu nguvu na kuzuia mwili kupata magonjwa hatarishi. Kutokana na matunda hayo kuwa na utajiri wa vitamini C nyingi iliyomo katika limao na ndimu ni siri ya faida za tunda hili. Pia ndimu ina vitamini B-complex, madini ya Kalsiamu, chuma, magnesiamu na potasiumu na fiba.

Kunywa maji peke yake (yasiyo na kitu) wakati wa asubuhi huwapa tabu baadhi ya watu,wengine hupata kichefuchefu, lakini kwa mchanganyiko huu inaongeza hamu na kumpa mtu raha ya kipekee .

Kuna faida nyingi ambazo utazipata pale ukinywa maji yenye ndimu au limao, ambazo ni kama zifuatazo.

**Huchochea mmeng'enyo wa chakula tumboni**

Maji yenye ndimu husaidia chakula kusagika vizuri na haraka katika mfumo wa chakula.

Pia maji ya uvuguvugu husaidia kusawazisha utumbo uliojikunja na kutoa mawimbi tumboni na kufanya chakula kusukumwa vizuri.

**Huboresha Kinga za Mwili**

Vitamini C na potasiumu iliyomo kwa wingi katika limao inasaidia katika utengenezaji wa seli za kinga katika mwili.

**Unyonywaji wa Madini Mwilini**

Vitamini C iliyomo katika limao husaidia kunyonywa kwa madini mwilini hasa madini ya chuma ambayo ni muhimu kwa utengenezaji wa damu. Hata kama maji ya ndimu yakiwa baridi.

**Kinga Dhidi ya Saratani**

Vitamini C ni antioksidant (antioxidant) ambayo inasaidia kuondoa mionzi hatari mwilini ambayo imetambulika kusababisha saratani.

**Kupunguza hatari ya kiharusi**

Kutokana na matokeo ya kitafiti, ulaji wa matunda jamii ya limao( HYPERLINK "http://en.wikipedia.org/wiki/List_of_citrus_fruits" \t "_blank" citrus fruits) inasaidia kupunguza hatari ya kupatwa na shambulio la kiharusi aina ya ischemic( HYPERLINK "http://www.mayoclinic.org/ischemic-stroke/img-20009031" \t "_blank" ischemic stroke) hasa kwa wanawake.

**Usafishaji wa mwili na damu**

Limao husaidia kusafisha damu kwa kuondoa uchafu. Limao pia husafisha figo, ini na mfumo wa chakula.

**Kurekebisha sukari katika mwili**

Limao husaidia kuweka kiasi cha sukari tumboni na katika mwili kuwa katika kiasi stahili.

Hii inawasaidia sana wagonjwa wa kisukari katika ulaji wao.

**Dawa ya Kikohozi na Mafua**

Limao ikitiwa katika maji ya uvuguvugu na asali hutibu mafua na kikohozi kwa njia ya asili.

**Urekebishaji wa ngozi na kupona makovu**

Limao inasaidia kufanya ngozi isizeeke. Kama unataka kubaki kijana basi limao litakusaidia.

Tabia za vitamin C za kusafisha uchafu zinasababisha kufanya ngozi kuwa na afya na kutozeeka haraka.

**Kupungua uzito**

Limao hupunguza hamu ya kula, hivyo kuepusha kukabiliana na tatizo la uzito mkubwa kutokana na kula chakula kingi bila mpangilio.

Limao litakufanya ujisikie kushiba muda mrefu hivyo kusaidia wale amabao wanataka kupungua uzito.

**Kuondoa Harufu Ya Mdomo**

Limao husaidia kuua bakteria wabaya mdomoni ambao husababisha harufu mbaya.

Ni zoezi rahisi na haraka kabisa, weka maji yenye joto kidogo (vuguvugu) katika glasi au kikombe, kata limao au ndimu vipande viwili na kamua kipande kimoja tu ndani ya glasi yenye maji.

Kunywa na uanze siku mpya. Ni vizuri ukafanya hivi dakika 30 kabla ya kula chochote kwa ajili ya kupata faida zaidi.

Anza leo kwa kunywa maji yenye ndimu kila siku asubuhi na uone mabadiliko ndani ya mwili wako.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Theddy ashauriwe kurudi nyumbani kumenoga



Na Joseph Kulangwa

UKISIKIA habari kuwa kuna binti Mtanzania anamshauri rais wa nchi nyingine, unapata hisia gani? Unajiuliza nini au unapata picha gani? Bila shaka picha inayokuja ni ya binti mwenye akili sana, binti mwenye staha iliyopitiliza, lakini mwenye weledi uliotukuka.

Lakini utabaki na maswali ya kwa nini sisi hatukumwona mpaka tukamwacha akaenda kushauri Rais wa nchi nyingine wakati nasi tunaye Rais ambaye pengine hana mtu wa aina hiyo, mshauri wa masuala ya mawasiliano!

Theddy Ladislaus ana umri wa miaka 29 tu, lakini ni Mshauri wa Mawasiliano ya Kimkakati wa Rais Edgar Lungu wa Malawi tangu mwaka 2016. Tulizoea kuona wazee ndio wanakuwa washauri wa marais. Tunamkumbuka marehemu Kingunge Ngombale-Mwiru, akiwa mshauri wa Rais Jakaya Kikwete.

Tunamkumbuka Profesa Ibrahim Lipumba, akiwa mshauri wa Rais Ali Hassan Mwinyi baada ya kuifanya kazi hiyo Uganda akimshauri Rais Yoweri Museveni kwa kipindi krefu tu.

Ni jambo la kujivunia, kwamba tuna binti huyo ambaye si tu anaipa sifa familia yake, lakini pia nchi yake ya Tanzania, kwamba kumbe inaweza kutoa washauri wa aina hiyo kwa viongozi wa mataifa mengine.

Theddy pamoja na kumshauri Rais Lungu, alishakuwa mshauri pia wa Makamu wa Rais wa Ufilipino, Jejomar Binay mwaka 2014, pengine Rais Lungu alipomwona au kumsikia akaomba apate pia huduma yake hiyo.

Ni mtaalamu wa kushauri viongozi na kampuni, na taaluma hiyo aliipata Ulaya, hivyo kazi yake anaijua vizuri na ndiyo sababu sasa anatumika katika nchi ya kigeni, tena katika Ikulu ya nchi hiyo.

Mhitimu huyo wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, mwaka 2014, alishauri pia viongozi wa juu na serikali katika nchi za Nigeria, Ghana na Amerika Kusini.

Kwa mujibu wa kazi yake, ni kwamba mawasiliano ya kimkakati ni yanayofikisha ujumbe kwa wakati, akifafanua kuwa kwa mujibu wa mfumo, kabla hujawasiliana lazima kupima mambo mbalimbali.

Kwamba je, huu ni muda wa kuongea au kunyamaza na kama ni kuongea ni kwa mantiki ipi, akitolea mfano wa msiba wa Rais Dk John Magufuli, kwamba ni jinsi gani tukio kama hilo linapaswa kufikishwa kwa umma.

Majukumu ya Theddy ni ya kuunganisha serikali na wananchi, kuhakikisha wanajua serikali yao inafanya nini wakati gani, na hiyo inatakiwa kufanyika haraka bila kuacha nafasi ya watu kuchomekea yao.

Kwa kifupi, Theddy anasema linapotokea jambo, mara moja lipimwe kwa muktadha na kasi ya kuwasilisha kwa wananchi bila kusababisha athari hasi kwa jamii husika.

Katika jamii kuna upotoshaji wa mambo kupitia mitandao ya kijamii, ambayo inabeba mambo mengi, hivyo kuwa na watu aina ya Theddy kunaleta tija sana katika serikali na jamii kwa jumla.

Kashfa au upotoshaji unapotokea kupitia mitandao ya kijamii, kunatafutwa jinsi ya kujibu kwa ama kukanusha au kurekebisha kilichozungumzwa. Hilo linahitaji mtu mahiri kama Theddy.

Tujiulize, Tanzania tunao watu wa aina hiyo wangapi? Au tunawasomesha na kuwaacha watafute malisho mema nje ya nchi! Watu aina hii wanatakiwa kuwapo Ikulu sasa, ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan.

Hiki ni kipindi ambacho kina maneno mengi, watu wamegawanyika pande mbili, wapo wanaomwunga mkono Rais Samia, lakini wapo wanaompinga huku wakionekana, kuendelea kumuunga mkono marehemu Dk John Magufuli. Hivyo vinenoneno ni vingi.

Kama inawezekana kwa nini Rais Samia asimwombe Theddy huko aliko arejee nyumbani ambako kumenoga, ili amsaidie katika Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, na amwache Gerson Msigwa akasimamie Idara ya Habari, MAELEZO, kikamilifu.

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Walimu vijana wanaikosea heshima taaluma ya ualimu

MWANADAMU ni zao la jamii yake. Wanasaikolojia wanaamini kuwa namna anavyotembea, anavyokula, anavyoamini, anavyovaa, anavyowasiliana, ni matokeo ya watu waliomzunguka.

Kwamba ukiacha sababu za kibaolojia, mazingira yana mchango mkubwa katika kuumba tabia tulizonazo. Mfano; asilimia kubwa ya waliozaliwa katika familia za Kiislamu au Kikiristo, huwa hawana sababu za moja kwa moja zilizowavuta katika imani hizo.

Wengi walijikuta wakiingia huko kwa sababu tu walipozaliwa waliwakuta wazazi au ndugu zao wengine wakiwa waumini wa dini hizo.

Hapa nchini, serikali imekuwa ikilitambua hilo kwa kujaribu kuipa kipaumbele taalamu ya ualimu licha ya changamoto za hapa na pale. Walau juhudi zinaonekana.

Moja ya mapinduzi ya kuvutia katika taaluma hiyo ni uwapo wa walimu wengi wenye umri mdogo. Binafsi nimekuwa nikipendezwa na hilo, japo bado nautambua na kuuthamini mchango wa walimu wakongwe.

Nina sababu za kisaikolojia inayonifanya nivutiwe na uwapo wa walimu vijana katika shule zetu. Ukweli ni kwamba inaongeza hamasa (motivation) kwa wanafunzi wanaotamani kufikia mafanikio wakiwa katika umri mdogo.

> **Nina sababu za kisaikolojia inayonifanya nivutiwe na uwapo wa walimu vijana katika shule zetu. Ukweli ni kwamba inaongeza hamasa (motivation) kwa wanafunzi wanaotamani kufikia mafanikio wakiwa katika umri mdogo.**

Nikirejea katika kuyapa nafasi macho yangu kuona, nikiri wazi kuwa licha ya mvuto walio nao kwangu, lakini zipo aina za mavazi na mitindo ya nywele kwa walimu vijana katika shule nyingi, hasa za sekondari, ni changamoto kubwa isiyopaswa kufumbiwa macho.

Nikianza na walimu wa kike, wamekuwa kichefuchefu mbele ya jamii kwa mavazi ya nguo fupi au yanayobana, ambayo kwa kiasi kikubwa huyaanika maungo yao. Je, mwanafunzi wa kike anayevutiwa na mwalimu huyo anaandaliwa kuwa mtu wa aina gani katika jamii?

Hebu tujiulize, ikiwa tunapeleka watoto shule ili kuwaepusha na uhuni uliojaa mitaani, halafu anakutana na mwalimu wa aina hiyo, nini tofauti?

Walimu wa kiume nao ni tatizo linapokuja suala hilo la mavazi. Achana na suruali zao za kubana miguuni 'model', ambazo licha ya sasa kuonekana kuwa mtindo mpya, ukweli ni kwamba miaka michache iliyopita zilikuwa zikivaliwa na wanawake tu.

Lipo hili la kuingia darasani wakiwa wamevaa mlegezo (suruali chini ya makalio). Nimelishuhudia hilo mara nyingi na sina shaka kuwa hata wazazi wanaofika shuleni mara kwa mara kufuatilia maendeleo ya watoto wao wanaweza kukiri kama si kuniunga mkono kukemea upuuzi huo.

Aidha, walimu hao wamekuwa kituko zaidi katika mitindo yao ya nywele. Kama wafanyavyo vijana wenzao wa mitaani, nao wamekuwa wakinyoa staili za ajabu kana kwamba si watumishi wa umma, tena katika taaluma nyeti.

Mwisho, niulize, ni kweli kamati za shule haioni au zinafurahia uchafu huo? Kama jibu ni hapana, nini kimefanyika kukabiliana nao?

Niulize pia, kama kuna hatua wanazochukuliwa walimu hao kwanini tatizo linaendelea na kuchafua taswira na maana halisi ya shule?

Mbali na mitindo ya mavazi, nywele na namna ya kujiremba kwao, lakini pia lipo suala la utoaji wa adhabu, kundi hili la walimu vijana wao hawana maumivu ya uzazi na hii huenda inasukumwa na wengi wao kutokuwa na familia.

Ukiwakuta wanachapa mwanafunzi, kamwe hawaangalii mahali sahihi na salama pa kuchapa, wanachapa kama wanaponda nyoka.

Nalisema hili kwa uhakika kwa sababu macho yangu yamepata kuyaona matukio ya namna hii mara kadhaa kwenye shule za msingi na sekondari.

> **Walimu wa kiume nao ni tatizo linapokuja suala hilo la mavazi. Achana na suruali zao za kubana miguuni 'model', ambazo licha ya sasa kuonekana kuwa mtindo mpya, ukweli ni kwamba miaka michache iliyopita zilikuwa zikivaliwa na wanawake tu.**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

# Fahamu umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako

NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu. Ndoa sio taasisi ya kuivamia bali maandalizi yanayohitajika. Bahati mbaya sana, watu wengi huelekeza nguvu nyingi zaidi katika kuandaa sherehe kubwa za harusi, kuliko kujiandaa kuwa mume au mke bora. Matokeo yake, watu wengi wameingia katika ndoa wakiwa hawana ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi ya ndoa. Hali hii imesababisha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Upo umuhimu mkubwa kwa wanandoa na wanandoa watarajiwa kufahamu mahitaji na madai ya taasisi ya ndoa kabla na baada ya kuingia katika ndoa.

Maisha ni safari ndefu inayohitaji kujifunza na kukua kila siku. Kupata ufahamu mzuri kuhusu uhusiano wa ndoa ni zoezi la maisha yote ya wanandoa. Mtu anapooa na kuolewa afahamu kuwa anaingia katika shule ambayo haina kuhitimu. Hii ni hatua nyingine muhimu ya maisha ambapo uvumilivu unahitajika sana. Mungu alianzisha taasisi hii ili watu waingie, waipende na kuifurahia.

Hata hivyo, mambo yamekuwa kinyume kwa baadhi ya wanandoa. Wanandoa wengi wameshindwa kuishi maisha ya ndoa. Maisha ya ndoa ya baadhi ya wanandoa ni kama jangwa, ambapo muda wote hufukuta joto na kutimua vumbi. Wengi wao wamekuwa wanaharakati zaidi kuliko kuwa walezi wa ndoa zao. Usanii (Pretendence) unazidi kuongezeka katika ndoa nyingi. Wakiwa mbele ya watu wengine hujifanya wako sawa na wanapendana, lakini maisha yao ya ndoa yamejaa migogoro na kutokuelewana. Hali hii imesababisha wanandoa wengi kupoteza hisia chanya na mvuto dhidi yao.

Lengo la makala hizi katika darasa hili la ndoa ni kuwasaidia wanandoa kuishi maisha bora ya ndoa. Unapojifunza usijitazame wewe tu, bali angalia familia yako pia. Kama una mtoto wa kiume ujue una mume wa mtu mtarajiwa. Kama una binti, basi ujue una mke wa mtu mtarajiwa. Mafunzo haya yatakusaidia kuweka misingi bora ya maisha ya baadaye ya watoto wako pia, kwani watoto hujifunza sana kutokana na matendo ya wazazi wao. Pia, mafunzo haya yamekusudia kuwapatia ufahamu na maarifa vijana wanaotarajia kuingia katika ndoa ili wawe waume na wake bora.

> **Kama una binti, basi ujue una mke wa mtu mtarajiwa. Mafunzo haya yatakusaidia kuweka misingi bora ya maisha ya baadaye ya watoto wako pia, kwani watoto hujifunza sana kutokana na matendo ya wazazi wao. Pia, mafunzo haya yamekusudia kuwapatia ufahamu na maarifa vijana wanaotarajia kuingia katika ndoa ili wawe waume na wake bora.**

Ni muhimu kuruhusu fahamu zetu kuingiza jambo jipya kwa kuwa kila siku ni ya kujifunza. Kujifunza huondoa kasumba ya kuishi kwa mazoea, hivyo, watu wapende kujifunza na kuruhusu mabadiliko ndani yao. Katika makala ya leo, tunajifunza umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako. Kupata muda wa kumsikiliza mtu mwingine ni zawadi ya thamani. Watu wengi wanajua kuongea, lakini watu wachache wanajua namna ya kusikiliza watu wengine. Mara nyingi watu wana shughuli nyingi kiasi cha kushindwa kusikiliza watu wengine. Kumsikiliza mwenzi wako ni muhimu kwani zipo faida nyingi.

Faida na umuhimu wa kumsikiliza mwenzi wako

- Kusikilizwa ni sehemu ya tiba kwani mtu anapata fursa ya kueleza ya moyoni mwake.
- Unapomsikiliza mwenzi wako unampa ujumbe kuwa unajali.
- Kusikiliza kunakusaidia kuwa karibu na mwenzi wako kimwili na kihisia.
- Unapomsikiliza mwenzi wako unajifunza zaidi kutoka kwake.
- Kusikiliza kunawasaidia wanandoa kufahamiana zaidi. Mwenzi atafahamu kile mwenzake achofikiri, mahitaji yake, hisia zake na matamanio yake.
- Kusikiliza ni ishara ya kumheshimu mwenzi wako.
- Unapokuwa msikilizaji mzuri wa mwenzi wako, unatoa ujumbe wenye kuonesha kuwa yeye ni mtu muhimu.
- Kumsikiliza mwenzi wako huongeza pendo, mahaba na mvuto.

Kwa hiyo, usimpuuzie mwenzi wako, bali tamani kumsikiliza. Jihadhari na mambo au vitu vinavyoweza kukufanya ukose muda wa kumsikiliza mwenzi wako, kwani baadhi ya wanandoa simu za kiganjani au kazi zimechukua muda wa wenzi wao na watoto. Ni muhimu kukumbuka kuwa, upo kwa sababu watu wengine wapo! Dhamiria kupata muda wa kumsikiliza mwenzi wako, halikadhalika na watoto wako pia. Usipende wewe usikilizwe tu, lakini tamani kusikiliza mtu mwingine pia. Unaposikiliza unajitengenezea mazingira ya wewe kusikilizwa pia. Kusikiliza ni jukumu la msingi la upendo katika ndoa. Zingatia hii itakusaidia katika maisha ya ndoa na kuongeza thamani yako kwa mwenzi wako!

**•Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

MEI 16, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 10


**Wazazi wasitafute mchawi mtoto kibaka**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Pendezesha nyumba yako kwa bustani ya mboga



KIPUPWE

## Utakavyojiepusha kukauka ngozi, midomo

Ukurasa 14

# Wazazi wasitafute mchawi mtoto wao kibaka

Na Beatrice Moses



MWENYEZI Mungu mwingi wa rehema, anakirimia mema mengi ikiwamo kuwa na watoto ambao dhamana ya kuwalea ipo mikononi mwa kila mzazi.

Watoto wanapaswa kulelewa kwenye maadili yaliyo mema yanayompendeza Mungu .

Mazingira ya malezi ya sasa yakuwa yenye maswali mengi kutokana na tabia zinazoonyeshwa na baadhi ya watoto na hata vijana.

Ukianzia kwenye mwenendo wao hadi mavazi na lugha wanazozitumia kwenye mazungumzo yao yanatia ukakasi kuyasikiliza.

Uwezekano wa kuwa malezi ya vijana hawa ndiyo yamesababisha wawe na tabia zinazosababisha maswali mengi, baaadhi wazazi wanastahili kunyoshewa vidole kwa kwa wamechangia hali hiyo kutokana na kujisahau au kutotambua wajibu wao kwenye malezi ya watoto.

Mzazi asiyekuwa na hofu ya Mungu, huyu ni wazi kuwa ni chanzo cha kuharibu mmomonyoko wa maadili kwa mtoto hatimaye vijana, kwa kuwa mwalimu wa kwanza kwa mtoto ni mzazi ama mlezi.

Hata nchini dini kubwa zinazojulikana ni Ukristo na Uislam, ambapo kwa kiasi kikubwa kuna mambo kadhaa wanashabiana hasa kutokana na baadhi ya vitabu vyenye habari za manabii na mitume waliopo kwenye agano la kale ikiwamo za kuhusu Ibrahimu,Musa na Yusufu.

Hiyo inajidhihirisha hata kwenye majina siyo ajabu kukuta baadhi ya majina yapo pande za dini zote mbili, ambazo zinahimiza kumcha Mungu kwa uaminifu, kuna mambo kadhaa ambayo yameelezwa kwenye vitabu hivyo yanayotoa mafunzo jinsi manabii na mitume hao walivyofanikiwa na kubarikiwa kwa kumcha Mungu.

Ibrahimu aliishi miaka mingi alibarikiwa na Mwenyezi Mungu kutokana na jinsi alivyokuwa anamheshimu, kwa kifupi ni kwamba vitabu hivyo vinatoa mafunzo jinsi ambavyo kumcha Mungu kuna baraka kubwa na wale ambao hawakumheshimu waliishi maisha yenye laana.

Kuna wazazi wao hawajishughulishi kabisa kumcha Mungu, wanapenda anasa na starehe kwenye nyumba za ibada hawaonekani, katika mazungumzo yao muda mwingi wanatumia lugha zisizo na staha, watoto wanazisikia hivyo nao wanazibeba na kuzitumia kwa wenzao wakiwa shuleni au kwenye michezo yao.

Kuna baadhi ya watoto ambao wamefukuzwa shule kutokana na tabia zao kuwashinda walimu, miongoni mwa tabia hizo ni pamoja na wizi, ukorofi na kutumia lugha chafu dhidi ya wenzao.

Kwenye baadhi ya shule za mabweni wizi ni mkubwa ndiyo maana wanafunzi wanahimizwa kuwa na masanduku ya chuma, ambayo bado nayo huwa si salama kwani vijana hao waliolelewa vibaya huvunja makufuli na kuiba vitu, wengine wanaiba nguo za wenzao zilizoanikwa kwenye kamba.

Wazazi wenye hofu ya Mungu waendelee kuwalea watoto katika misingi mizuri ili wasisombwe na wale ambao wamelelewa na wazazi wasio na hofu na Mungu, wahimizwe kuzingatia mafunzo mema wanayopewa na walimu wao kwenye nyumba za ibada.

Jamii inatamani kuwa na vijana wenye tabia njema ambao hawajengi hofu kutokana na kuwa na tabia za uovu, mtoto akijua kumcha Mungu hawezi kushawishika kuiba, kutukana ama kujeruhi wenzake kwa vipigo ama kushiriki vitendo vya ngono, maana kumcha Mungu ni mwanzo wa hekima.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**La formation du pluriel – Muundo wa sentensi zenye wingi. Zingatia!**

Charles (ms) estgrand et élégant. Ses frères (mp) sontégalementgrands et élégants – Charles ni mrefu na maridadi. Kaka zake pia ni warefu na maridadi.
Caroline (ms) estsportive et intelligente. Sessœurs (mp) ne sont pas du tout sportivesmais ells sonttrèsintelligentes – Caroline anapenda michezo na ana akili. Dada zake hawapendi kabisa michezo lakini wana akili.

**Je suisheureuxquandtousmesamissontheureux! – Nina furaha pindi marafiki zangu wote wakiwa na furaha!**
Joyeuxanniversaire! Voiciungrandcadeau et grosbisous! – Heri yasiku ya kuzaliwa! Nakupa zawadi **kubwa** na busu **kubwa!**

**Muhimu:** (ms) – masculinsingulier = jinsia ya kiume katika umoja. (mp) – masculinpluriel = jinsia ya kiume katika wingi.


**Weka maneno yafuatayo katika wingi.**
Grand……………………………………
Élégant…………………………………
Sportive…………………………………
Intelligente……………………………
Heureux…………………………………
Gros………………………………………

**Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano.**
En vacances
Le temps est (agréable – agréables).
Le soleilest (chaud - chauds).
Le pays est (magnifique – magnifiques).
Les gens sont (gentil – gentils).
Les enfantssont (bruyant – bruyants).
L'appartementest (confortable – confortables).
La nourritureest (bonnes – bonne).
Les vacancessont (courte – courtes).
La vie est (belles – belle).
Les habitants sont (accueillants – accueillant).
Les problems ne viennent pas (seuls – seul).
Le parfum sent (bons – bons).
Le president est (connu – connus).
La filleest (méchante – méchantes).
La musiqueest (anglaise – anglaises).
La voitureest (japonaises – japonaise)
Cetteréférenceest (pertinente – pertinentes).
Le socialismeest (mourants– mourant).
Les livressont (bons – bon).
La porteest (ouvertes – ouverte).
Le portailest (ouverts – ouvert).
La boutique est (fermées – fermée).
La vie est (faciles – facile).
La soirée est (dansante – dansantes).
La journéeestassez (longues – longue).
Les basiquessont (dures – dure).
La méchancéteest (graves – grave).
La nuitest (courtes – courte).
Andika sentensi zifuatazo katika wingi.

Le texteestdifficile.

## WATOTO

## PAKA RANGI




CHEKA

Alichokifanya daktari

JAMAA mmoja ambaye ni mara ya kwanza kutembelea mjini, aliwaacha watu hoi kwa kicheko baada ya kupelekwa katika kibanda cha kununulia koni.

**Mama:** Ebu nipatie koni mbili ya kwangu na huyu ndugu yangu

**Jamaa:** Duu, chakula gani hiki mbona kama kokonoko wa kule shambani, ila huyu ana rangi nzuri

**Mama:** Hapana hii ni koni

**Jamaa:** Tafadhali mama siwezi kula, bora uninunulie togwa

**Mama:** Sema taratibu unanitia aibu.

**SWALI**
Tabia za binadamu zinakaribiana na mnyama gani wa porini?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unapoizoea tabia fulani unaihalalisha pasipo kujua, kisha inakuangamiza!

***KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii. Wiki iliyopita nilijadili binti aliyejikuta katika maisha ya ukahaba kwa kuvutwa na rafiki. Alianza taratibu kisha akazoea, akahalalisha maisha asiyotarajia. Hebu leo nichambue kidogo roho ya mazoea inavyotesa watu.***

Kinachowasumbua sana watu wengi ni roho ya mazoea. Kuna vitu ambavyo tunavihalalisha, kisha tunaanza kuvizoea pole pole wakati hatupaswi kuvizoea. Kuna vitu katika maisha yetu msomaji wangu hatupaswi kuvizoea hata kidogo kwa sababu ukivizoea vinakuletea madhara fulani.

Vipo vitu ukivizoea vitaharibu kabisa maisha yako ya kiroho. Yaani ukivizoea, ukaanza kuvifanya hutaweza kuona matokeo ya papo kwa papo. Lakini kadiri siku zinavyokwenda, utaanza kuona taratibu unazidi kuanguka na pia kupata madhara ya kiroho na kimwili.

Ndama, yaani mtoto wa ng'ombe, hawezi kuzoea nira. Unajua nira ni kifaa anachovalishwa shingoni wale ng'ombe wanaolima, halafu jembe linapitishwa katikati. Hiyo inaitwa nira.

Kwa hiyo, ndama ambaye hajazoea ni mchanga. Ukijaribu kumfunga hiyo nira anaumia. Hivyo, kwa hali yoyote ile hawezi kuzoea. Ukitaka ufanikiwe kwenye maisha yako au unapotaka uende kwenye hatima yako, kuna vitu hupaswi kuvizoea.

Hiyo ni kutokana na ukweli kwamba unapovizoea tayari unavihalalisha. Kuzoea ni kuhalalisha. Wapo watu wengi walianza kuzoea vitu fulani ambavyo vimeua kabisa hatima zao. Vipo vitu usithubutu kuvizoea hata kama wengine wataanza kuvizoea, wewe kataa. Waambie mimi siwezi kuzoea.

Kwa mfano, mwambie mwenzako Mungu siwezi kumzoea, kwenda nyumba za ibada siyo kwa mazoea. Nimeeleza kuwa vipo vitu ukivizoea vitakuharibia maisha yako ya kiroho. Kuna watu walishuhudia kuwa walikuwa moto katika kumcha Mungu, kufanya kazi maofisini hata kupata ufanyakazi bora, lakini leo moto ule umezimika. Kisa roho ya mazoea imewashusha ari.

Wengine hawaoni zile ndoto nzuri za zamani. Ni kwa sababu kuna vitu walianza kuvizoea pole pole. Shetani anachofanya ni kukuletea vitu fulani ambavyo zamani ulikuwa unaviogopa, unavikimbia. Mfano, kuna dhambi ulikuwa unaikimbia kabisa, hata kuiangalia wala kusikia hutaki. Lakini leo umeanza kuizoea taratibu na kuanza kuihalalisha.

Siku zote shetani hawezi kukushinda, ni lazima akuletee vitu utaviona ni vya kawaida kumbe ni sumu tamu. Kuna sumu unaweza ukaila leo, ikakuua baada ya miaka 10. Nyingine ukalishwa leo, ukafa baada ya mwaka mmoja.

Shetani leo anaachilia vitu kama ni vitamu vile, lakini vinakuua. Ni kama vitu vitamu, lakini ni dhambi. Anakushawishi kwenda kwenye tukio fulani, huku akikuaminisha hakuna tatizo, kumbe unajilengesha kwenye bomu la nyuklia.

Watu wengi wanauliwa kiroho kwa sababu ibilisi anawaletea sumu tamu. Mwanafunzi anadanganywa na shugadadi, anarubuniwa kwa simu ya kiganjani inakuwa ni sumu kwa ndoto yake kielimu.

Yapo mambo hutakiwi kabisa kuyazoea ili kuepuka kujihalalisha. Pale unapoyahalalisha na Mungu anakaa pembeni. Siku zote jitahidi kutobadili mwelekeo wako. Sema siwezi kuzoea umasikini, siwezi kuzoea ugonjwa, kataa maana siyo sehemu ya maisha yako.

***Mpenzi msomaji, niishie hapa kwa leo ili nikupe muda kutafakari ujumbe katika makala haya. Je, una maoni au kisa cha kimaisha ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Kilio ukosefu dawa, maji kikubwa kitatuliwe kwa vitendo

KILIO cha wawakilishi wa wananchi dhidi ya huduma muhimu za kijamii kama maji na afya ni kikubwa, na kila aliyesimama kuchangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ametaka jitihada za makusudi.

Kwenye afya kilio ni ukosefu wa dawa kiasi cha wananchi walio na bima kulazimika kusafiri umbali mrefu wa nauli ya Sh. 10,000 kufuata dawa za Sh. 3,000.

Jumla wa wabunge 40 waliochangia hoja 57 ikiwamo 35 kwa kuzungumza na watano kuandika hoja zao katika Wizara ya Afya, na wachache sana waligusia suala la Corona.

Kila mbunge alionyesha kuna tatizo kubwa sekta ya afya kuanzia ngazi ya vijijini, na licha ya kuwa na kadi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (ICHF), bado walielekezwa kununua dawa.

Wapo ambao walisema mwananchi anasafiri umbali mrefu kutoka kijiji kwenda mjini kununua dawa, na wale wanaokwenda kwenye maduka maalum ya kupata dawa kwa bima wanapata usumbufu mkubwa.

Kilio hiki ni kikubwa kwa kuwa afya za watu ni muhimu sana, ili tuwe na taifa imara la wachapakazi lazima nguvu kazi ya kutosha iwepo na yenye afya tele. Wapo walioeleza jinsi wazee, wajawazito na watoto wanavyosota kupata matibabu bure licha ya sera kueleza kuwa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali kutakuwa na dirisha maalum la kuwahudumia wazee.

Baadhi ya maeneo wanahudumiwa katika dirisha husika, lakini wanapaswa kuchangia matibabu na wanakosa dawa jambo linalowaumiza wengi.

Mbunge kutoka Tabora alieleza katika hospitali moja wajawazito wakijifungua mtoto wa kiume wanatozwa 50,000 na wakike 40,000, huku watoto chini ya miaka mitano wakitozwa fedha licha ya serikali kusema makundi hayo yatapata huduma bure.

Wengi walisema upatikanaji wa dawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD), siyo wa kuridhisha kutokana na deni ya serikali, huku dawa nyingi zikikosekana.

Kilio kinachofanana na hicho ni upatikanaji wa maji katika maeneo mengi nchini kiasi cha wengi kunywa maji machafu, na hata ile nia ya kufikia asilimai 80 mijini na asilimia 73 vijijini kushindwa kufikiwa.

Wengi walilia mkwamo kwenye miradi mingi ya maji na kutaka serikali kuongeza jitihada na bajeti ya maji kwa kuwa lina uhusiano wa moja kwa moja na afya za watu. Naungana na wabunge hawa kuwa upo uhusiano wa moja kwa moja baina ya upatikanaji wa maji na afya za watu, mathalani kwenye magonjwa ya mlipuko na kuhara.

Nia ya kumtua ndoo mama kichwa ili kuepuka muda mwingi unaopotea kutafuta maji ambao ungetumika kwenye uzalishaji haijatimia, au kuhakikisha upatikanaji wa maji umbali usiozidi mita 400.

Katika majumuisho ya wizara zote serikali iliahidi kufanyia kazi hoja za wabunge ikiwamo kuongeza kasi ya usambazaji maji na upelekaji wa dawa ikiwamo kulipa deni ya MSD.

Iwapo haya yatatekelezwa na kusimamiwa vyema bajeti iliyopitishwa na Bunge maana yake mwakani katika mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hizo malalamiko yatakuwa yamepungua, badala ya

> **“Kwenye maji kilio kingine kilichozua mvutano ni upotevu wa maji ambao kwa miaka minne umeisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. milioni 332 ambazo zingetekeleza miradi mingine.**

wabunge kutoa kilio itakuwa ni pongezi.

Ni muhimu sana bajeti za wizara hizi zikasimamiwa vyema, kuwe na ufuatiliaji wa kila Shilingi inayotolewa kuhakikisha inafanya kilichokusudiwa, ikiwamo kuziba mianya yote ya upotevu wa dawa, lakini fedha zipelekwe kwa wakati.

Kwenye maji kilio kingine kilichozua mvutano ni upotevu wa maji ambao kwa miaka minne umeisababishia serikali hasara ya zaidi ya Sh. milioni 332 ambazo zingetekeleza miradi mingine.

Hakuna ubishi kuwa upotevu wa maji upo na mathalani kwa jiji la Dar es Salaam ni kawaida kukuta mabomba yanamwaga maji ovyo, ambayo yangetumiwa na wananchi ambao wanakosa huduma hiyo kwa sababu tu ya uchache wa maji.

Naamini bajeti ya mwaka 2022/23 itakuja na majibu kwa kiasi gani matatizo yameshughulikiwa na sasa afya kwa wote inakwenda vizuri sambamba na upatikanaji wa dawa, huku ukosefu wa majisafi na salama kwa mijini kuwa asilimia 90 na vijijini 80, hali ambayo itapunguza gharama za kutibu magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa maji.

# HARUSI





Ilikuwa furaha ya aina yake wakati Elisha Mgendi na Adelina Kiondo, walipofunga ndoa Aprili 25 mwaka huu, katika Kanisa la Wasabato mkoani Morogoro





# MITINDO





LIKABILI BARIDI

## Pigilia nguo hizi, utaniambia

KILA mwanamke anajitahidi kuwa na mwonekano wa kuvutia kila wakati. Katika msimu huu wa baridi kuna aina nyingi ya mavazi ambayo husaidia kumpatia mtazamo mzuri zaidi.

Wabunifu wa mavazi wanakuwa makini kutengeneza nguo ambazo zitakidhi kiu ya watumiaji wao hasa katika kuwapatia joto la asili na pia kuonekana tofauti.

Haya ni mavazi ambayo yanatamba katika msimu wa kipupwe wa mwaka 202.

### NGUO ZA KNITTED

Ni aina ya magauni ambayo yametengenezwa kwa kutumia pamba nzito na Hariri, licha ya kumtoa vizuri mwanamke pale anapovaa, pia humpatia joto la asili na kumfanya ajimiamini zaidi.

### NGUO ZA VELVET

Ni nguo nzuri katika majira ya baridi kwa ajili ya wanawake,imetengenezwa kwa mitindo tofauti na kumfanya mtumiaji kuwa na chaguo lake.

Jambo zuri ni kwamba nguo hizi zinaruhusu kuvaa na kofia na ukatoka bomba.


### NGUO ZA LUSTER


Sawa na nguo za aina ya Jaketi, lakini hizi zimekuwa na mishono tofauti ambayo hufanya mavaaji kuwa tofauti na mwenye furaha.

## UREMBO









KIPUPWE

# Utakavyojiepusha kukauka ngozi, midomo

KATIKA kipindi cha baridi kali cha kipupwe, watu wanapata changamoto kubwa ya utunzaji wa mwili kutokana na msimu huu ngozi huwa kavu na inayokakamaa na midomo inapasuka.

Kimsingi kipindi kinakuwa kigumu hasa kwa wanawake wanaopenda urembo na kila wakati wanataka kujiona wana furaha zaidi.

Lakini si jambo la kuogopa sana, kwani ukizingatia mambo muhimu ya kufanya unaweza kukabiliana na hali hiyo na hatimaye ukaendelea kuwa na ngozi laini na yenye afya.

**MAJI YA KUTOSHA**

Kutokana na hali ya baridi, kiwango cha unywaji maji hupungua. Hata hivyo, unatakiwa kuendelea na tabia ya kunywa maji ya kutosha ili kuufanya mwili kuwa na unyevunyevu.

Ili kuongeza hamu ya kunywa, unaweza kuweka ladha mbalimbali kama limao au chungwa.

**ACHA KUSACRABU**

Wakati wa kipupwe ngozi inapoteza unyevu kwa urahisi, hivyo epuka 'kusacrub' uso kwani utaongeza ukavu na kujisikia tofauti.

Mara nyingi tumia mafuta ya kulainisha uso ili ngozi isitoe mikunjo. Na endapo utafanya 'scrub' yako, tumia maski ili kurudisha uhalisia wa ngozi yako.

**'CREAM' YA MIKONO**

Kwenye mkoba wako hakikisha unakuwa na Cream ya kusafisha mikono, mafuta haya yatakusaidia kulainisha ngozi ya mikono ambayo kwa kawaida kipindi hiki inakuwa kavu na ngumu.

Pia paka mafuta ya kulainisha midomo ambayo haiwezi kuhimili baridi na kusababisha ipasuke.

Ni hatari kulainisha midomo kwa kutumia mate kwani wakati mwingine husababisha vidonda.

**PUMZIKA VIZURI**

Kama hauna shughuli muhimu za kufanya, muda mwingi tumia ukiwa nyumbani ili kuepuka ngozi kukabiliana na baridi. Wakati wa kulala usiache kujipaka mafuta kwa sababu ngozi yako inajitengeneza vizuri usiku.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Kuoka keki ya Chocolate

KWA wale waliozea kula vitamu leo katika safu yetu yapishi tutaelekezana kwa pamoja namna ya kuipika keki ya chocolate.

**MAHITAJI**

Unga wa ngano vikombe viwili, sukari vikombe viwili, cocoa robo tatu ya kikombe na baking powder vijiko vya chai viwili .

Mahitaji mengine ni baking soda kijiko kimoja na nusu cha chai, 'espresso powder' kijiko kimoja cha chai, maziwa kikombe kimoja, mafuta nusu kikombe, mayai mawili, chumvi kijiko kimoja na na maji ya moto kikombe kimoja.

**NAMNA YA KUPIKA**

Pasha oven joto na weka nyuzi joto 350, vyombo unavyotumia kuoka keki vipake mafuta kisha weka pembeni.

Weka unga, sukari, cocoa,





baking powder, baking soda, chumvi na espresso powder kwenye bakuli moja.

Changanya vizuri mpaka mchanganyiko uchanganyikane vizuri. Ongeza maziwa, mafuta na mayai kwenye mchanganyiko wa unga.

Changanya mpaka uchanganyikane vizuri na kungeza maji ya moto kisha changanya kwa dakika mbili.Weka mchanganyiko kwenye chombo cha kuokea, oka kwa dakika 30 mpaka 35.

Epua chukua toothpick choma katikati kujua kama keki imeiva vizuri. Ikiwa tayari iache kwa dakika 10 ipoe.

Itoe kwenye chombo cha kuokea kisha itakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa muda wowote.

Karibu ufurahie pishi lako la keki tamu.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Pendezesha nyumba yako kwa bustani ya mboga



NYUMBA ni mahali pa kuishi, lakini pia nafasi inayobaki inaweza kutumika kutengeneza bustani nzuri ya mboga.

Wengine hupendelea kutumia nafasi hiyo kutengeneza bustani ya maua, lakini kwa kuweka bustani ya mboga kuna faida mara dufu. Kwanza hupendezesha mandhari kama utakavyokuwa umepanda maua na pili inakuletea chakula na kukupunguza gharama ya kununua mboga.

Mboga unazopanda kwenye bustani yako unakuwa na uhakika nazo kwa sababu unazihudumia mwenyewe kwa kumwagilia maji yaliyo salama.

Katika kufahamu zaidi namna ya kutengeneza bustani ya mboga, nilizungumza na Gerald Maiko mtaalam wa masuala ya bustani ambaye anabainisha namna ya kutengeneza bustani hiyo.

Anasema mojawapo ni kutumia makopo yanayotumika kupandia maua kandokando ya nyumba, gunia la sandarusi kubwa au ndoo.

Anasema katika vifaa hivyo unachanganya humo udongo, pumba za mpunga au mbolea ya samadi iliyooza vizuri.

"Udongo utasaidia kuwezesha mmea kusimama, pia kuupatia virutubisho, lakini pumba zitasaidia mizizi kupita kwa urahisi na kuweka mazingira mazuri ya hewa, maji na mbolea ya samadi itasaidia kutoa virutubisho kwa mmea na kuvichanganya kwa utaalam.

Makopo yanayotumika kupandia mboga ni lazima yatobolewe chini ili kuzuia maji kubaki kwa wingi, na ndani yanatakiwa yawekwe pamba kwenye matundu yaliyotobolewa.

"Baada ya hapo unatakiwa kuweka udongo uliochanganywa vizuri kwenye makopo au ndoo, hapo utakuwa tayari umepanda mbegu zako ama mche wa mboga aina yoyote."

Kuhusu namna ya kuitunza anasema ni kuhakikisha unamwagilia angalau mara tu baada ya kupanda na kuendelea na kazi hiyo kutegemeana na aina ya mboga.

"Mboga kama sukuma wiki waweza vuna mara kwa mara, kazi yako ni kumwagilia tu. Unatakiwa kubadilisha udongo wako baada ya mavuno ili kuhakikisha mboga zako zina pata virutubisho vya kutosha."

Na namna ya kutengeneza bustani hiyo kwa kutumia gunia, Maiko anasema yenyewe pia inaweza kutengenezwa katika sehemu yoyote ya eneo la nyumba.

Katika gunia pia unaweza kuchanganya udongo, pumba na mbolea iliyooza.

"Zipo hatua mbalimbali za utengenezaji wa mboga kwa kutumia gunia, toboa gunia lako na ondoa kitako ili kuweka uwazi juu na chini, weka mti au ubao katikati ya gunia ukiuchimbia ardhini, kisha weka gunia lako katikati ya mti au mbao hiyo na lijaze kokoto."





"Weka udongo uliochanganywa vizuri kwenye gunia lako na baada ya hapo hakikisha kokoto zinabaki zikizungukwa na udongo. Weka gunia juu ya kokoto zilizozungukwa na udongo kisha lijaze na kokoto, rudia kujaza udongo ukilizunguka hadi kimo cha gunia hilo. Endelea kufanya hivyo hadi pale gunia lako litakapokuwa limejaa."

## Dondoo namna ya kupamba picha kuta za sebule yako

**1:** Chagua flemu ya picha ambazo zinaendana na rangi ya ukuta wa sebule. Hakikisha flemu inatosha ukubwa wa picha.


**2:** Pangilia kwa umakini picha zinazowekwa sebuleni, weka zile zenye furaha na kuleka matumaini kwenye familia.

**3:** Unaweza pia ukaweka picha za kisanii, kwa mfano, picha na asili, inayoonyesha anga ya bluu wazi au misitu wanyama pori. Pia picha za bustani na mandhari nzuri ya milima na mabonde zinaongeza uzuri wa sebule yako.

**4:** Ikiwa picha yako inavutia zaidi, unashauriwa kuweka sehemu ya pekee ili kutoa nafasi watu kuitazama bila kusumbuliwa na taswira zingine.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
SITOUKARIBIA WALA KUUGUSA 'MLUNGULA' HATA NIWE NA DHIKI YA KUFA
KIAPO
USHAWISHI
MKE WANGU HILO B#NG! NA HIYO 'BINDUKI' KWANI KUNA VITA?
ACHA LONGOLONGO KANIONESHE ALIYEKUFUNGIA KUANZIA IDI MOSI HADI LEO!
DEREVA STOP UCHEKIWE MANAKE SIKUKUU HAMKAWII KUUTWIKA
DUH! KAMANDA HACHEKI KAMA AMEFUNDA SUPA GRUU MDOMONI!
ACHEKE MFE?
HUU MZIGO UKIUTAZAMA KWA MACHO NI MWEPESI MNO!...
UONGO-ZII
SIKU HIZI WANAWAKE HAMPENDI PESA KABISA!
TUNAPENDA 'MIAMALA' ZAIDI
WEWE UNANIPA HELA YA NINI?
WAPIGA DILI
POLE POLE UTAJUA
SIKUKUU UKIJUMLISHA NA WIKIENDI JUMLISHA 'UKAPUKU'
SHANGWE ZA BIA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KAMA NDOTO ZAKO HAZIJATIMIA ENDELEA KULALA

## Watu 30 wahukumiwa kifo DRC

**KINSHASA,** DRC

WATU 30 wamehukumiwa adhabu ya kifo nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, baada ya kupatikana na hatia ya kushiriki katika vurugu dhidi ya polisi wakati wa sherehe za sikukuu ya Iddi mjini Kinshasa.

Wakili anayetetea vyama vya kiraia , Chief Tshipamba, aliliambia shirika la habari la AFP, kuwa watu hao walihukumiwa kifo katika shauri lililoanza juzi Ijumaa siku moja baada ya kutokea kwa machafuko hayo.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo haijawahi kutoa hukumu ya kifo tangu sheria ya kutoa adhabu hiyo ilipositishwa mwaka 2003.

Kuanzia kipindi hicho hukumu hizo hubadilishwa kuwa kifungo cha maisha jela.

**DW**

## Jaji Mkuu wa Iran atangaza kugombea Urais

JAJI Mkuu wa Iran aliyewahi kugombea kiti cha urais hapo nyuma, Ebrahim Raisi, ametangaza kugombea tena kiti hicho katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi unaokuja.

Kulingana na taarifa kutoka kwa chombo kimoja cha habari nchini humo, jaji huyo ambaye alikuwa hasimu wa rais Hassan Rouhani katika uchaguzi wa mwaka 2017, huenda atagombea mwaka huu.

Katika taarifa yake, Raisi alisema ameamua kugombea kutokana na matakwa ya watu wengi na ana nia ya kugombea kupitia chama binafsi ili alete mabadiliko katika utendaji na namna ya kuiendesha nchi.

Pia ameahidi kupambana na umasikini, rushwa, udhalilishwaji pamoja na ubaguzi iwapo atachaguliwa.

Ahadi hizo alizitoa miaka minne iliyopita wakati akigombea nafasi hiyo ya juu katika Jamhuri hiyo ya kiislamu.

Katiba ya Iran inamzuia Rais wa sasa Hassan Rouhani, kugombea muhula mwingine wa tatu madarakani.

**DW.**



Maroketi yaliyorushwa na wapiganaji wa Kipalestina yakipaa angani kuelekea miji ya Israel, wakati mgogoro kati ya pande hizo ukiendelea kushika kasi na kuaa zaidi ya watu 136 hadi jana. **(PICHA: DW)**

# Mapigano yaua Wapalestina 130, Waisraeli 9

**JERUSALEM,** ISRAEL

IDADI ya watu waliouawa kutokana na mashambulizi ya Israel dhidi ya Wapalestina katika Ukanda wa Gaza imefikia 132.

Hadi jana ilifahamika watu hao waliofariki, ambapo 32 kati yao ni watoto na 21 ni wanawake. Upande wa Israel iliripoti kupoteza watu tisa tangu mapigano yaanze siku ya Jumatatu.

Madaktari waliopo Ukanda wa Gaza, walisema watu saba waliuawa kufuatia mashambulizi ya anga ya jeshi la Israel katika eneo la kaskazini la Ukanda huo.

Wakaazi wa eneo hilo waliripoti pia taarifa za jeshi la wanamaji la Israel kurusha makombora kutokea Bahari ya Mediterenia.

Katika mitaa ya Ukingo wa Magharibi, wanajeshi wa nchi hiyo waliwauwa waandamanaji saba wa Kipalestina siku ya Ijumaa, wakati ghasia zikiendelea katika maeneo mbalimbali ya Israel, ambako raia wa Kiyahudi na Kiarabu wanapambana.

Milio ya ving'ora vya tahadhari ilisikika kwenye miji mikubwa miwili ya kusini mwa Israel asubuhi ya Jumamosi, baada ya Hamas kurusha makombora mengine kutokea Gaza.

Tangu mapigano kuanza siku ya Jumatatu, zaidi ya makombora 2,000 yamesharushwa kutokea Gaza kuelekea Israel, yakiwauwa watu tisa, mtoto mdogo mmoja na mwanajeshi na kujeruhi wengine 560.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linatazamiwa kukutana leo kujadili mapigano hayo yanayoendelea kati ya Israel na kundi la Hamas.

Waziri anayeshughulikia masuala ya Palestina na Israel kwenye serikali ya Marekani, Hady Amr, aliwasili nchini Israel siku ya Ijumaa kama sehemu ya juhudi za kupatanisha.

Msemaji wa wizara ya mambo ya kigeni ya Marekani, Jalina Porter, alisema Amr alitarajiwa kufanya mazungumzo na maofisa wa Israel na Palestina walioko Ukingo wa Magharibi, kusisitiza kusitishwa kwa mapigano.

Hata hivyo, Marekani haitaki kuzungumza na Hamas, inayodai ni kundi la kigaidi.

Hata hivyo, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, ambaye anatuhumiwa kuvitumia vita hivyo kujinufaisha kisiasa, hakuonyesha ishara yoyote ya kulegeza kampeni yake ya kijeshi dhidi ya Wapalestina.

Israel inasema imeshambulia maeneo takribani 800 ndani ya Ukanda wa Gaza, ikiwemo njia ya chini kwa chini inayotumiwa na wanamgambo wa Hamas.

Kufikia juzi, Israel ilikisia kuwa ilishafanikiwa kuwauwa zaidi ya makamanda 30 wa Kipalestina kwa mashambulizi yake.

Taarifa ya Umoja wa Mataifa ilisema wakazi wapatao 10,000 wa Gaza wamelazimika kuyakimbia makaazi yao.

**DW**

# Rais Malawi akasirishwa Bunge kumkataa mteule wake

**LILONGWE,** MALAWI

RAIS wa Malawi, Lazarus Chakwera, amekasirishwa na kitendo cha bunge kukataa kuthibitisha jina la mkuu wa kuongoza Ofisi ya Kupambana na Rushwa nchini humo. Akihutubia bunge hilo siku ya Jumatano, Rais Chakwera, alisema alisikitishwa na kukatishwa tamaa na kamati kukataa jina la mteule wake, Martha Chizuma, siku moja kabla.

Kamati ya Uteuzi wa Umma ya Bunge(PAC) ilisema Chizuma alikataliwa kwa sababu alishindwa kupata alama zinazohitajika kwa uthibitisho.

Nusu ya wabunge katika kamati hiyo walimpa alama za chini baada ya mahojiano ya tathmini, na matokeo yaliyokusanywa yalionyesha Chizuma alipata alama 15 tu kati ya 25 inayotakiwa.

Chakwera aliwataka wabunge waweke kando maslahi ya kisiasa na ya kibinafsi, badala yake wafanye sehemu yao katika kuharakisha mabadiliko ambayo Wamalawi wameyatafuta.

Tangu alipoingia madarakani mwaka mmoja uliopita, Chakwera ameendesha kampeni ya kupambana na ufisadi ambayo imepelekea watu kadhaa muhimu, akiwamo mshauri wa usalama wa Rais wa zamani Peter Mutharika, ambaye alikamatwa.

Chakwera anasema anaamini uteuzi wa Chizuma, anayejulikana kama iron lady utasukuma mbele lengo hilo. Chizuma, ambaye kwa sasa ni msimamizi wa masuala ya umma wa nchi hiyo, aliwaondoa maofisa wakuu watano kwenye nyadhifa zao kwenye kituo cha mdhibiti wa mawasiliano, akisema waliajiriwa kinyume cha sheria wakati wa utawala wa zamani wa Mutharika.

Mbunge Ashems Christopher Songwe, ambaye anatoka chama cha kiongozi huyo, alisema kwamba kuna madai wabunge wa upinzani walishawishiwa kupita kiasi kumkataa Chizuma.

## MAKALA

# Madaraka hayamfanyi mtu kuwa na akili zaidi



Na Magabilo Masambu

**Ukisoma maandiko matakatifu utagundua kwamba pamoja na nguvu alizonazo Mwenyezi Mungu, za kuumba na kutengeneza kila kitu katika ulimwengu huu, lakini bado inaonyesha hakutaka kuzitumia nguvu na uwezo wake pekee katika kukamilisha kazi ya uumbaji.**

MATUMIZI ya akili na nguvu ndiyo hutofautisha kati ya uongozi na utawala. Kiongozi bora hutumia akili zaidi kuongoza wakati mtawala hutumia nguvu zaidi kuliko akili kuongoza, japo wote kwa pamoja madaraka hayawapi akili zaidi.

Viongozi na watawala wengi mara nyingi hudhani kwamba madaraka huwapa akili ya kufahamu mambo zaidi kuliko wale wanao waongoza, dhana hii imewafanya wengi wao kukosea huku wakidhani wako sahihi katika maamuzi yao.

Uongozi ni jambo shirikishi, hata kama sheria itakuwa imekupa madaraka makubwa kiasi gani, lazima kutumia akili zaidi katika kuongoza badala ya kudhani kwamba unao waongozi hawana akili.

Utendandaji kazi wa mchwa, siafu, kumbikumbi, nyuki na wadudu wengine ungetosha kabisa kuwafanya viongozi wenye dhamana katika ofisi zao kujifunza namna bora ya kufanya kazi.

Hakuna namna kiongozi atafanikiwa bila kuwafanya wale anao waongoza kujiona sehemu ya uongozi wenyewe.

Ukisoma maandiko matakatifu utagundua kwamba pamoja na nguvu alizonazo Mwenyezi Mungu, za kuumba na kutengeneza kila kitu katika ulimwengu huu, lakini bado inaonyesha hakutaka kuzitumia nguvu na uwezo wake pekee katika kukamilisha kazi ya uumbaji. "Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu kwa sura yetu wakatawale samaki wa baharini na ndege wa angani na wanyama, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi" (Mwanzo:26)

Hii inadhihirisha kwamba uongozi unahitaji ushirikiano sijui Mungu alikuwa akiwaambia kina nani ili kumuumba mtu, lakini inaonyesha alikuwa akishirikiana na wengine. Maandiko haya pia yanaonyesha wazi kwamba wanyama, samaki, ndege wa angani pamoja na vitambaavyo juu ya nchi, ndivyo vinanyotakiwa kutawaliwa na hii ni kwasababu havina utashi. Binadamu haitaji kutawaliwa bali kuongozwa kwasababu anao utashi na akili.

Tabia ya kujifanya kiongozi unajua kila kitu inaweza kufunga milango ya kujifunza kutoka kwa wale unao waongoza na bahati mbaya jambo la uongozi ni kipawa sio elimu, unaweza kuwa Profesa bado ukawa mjinga katika maeneo mengi, kwasababu ni vigumu sana kujua kila kitu katika dunia hii.

"Watu walio hatarini sana ni wale ambao wanafikiri kuwa wanajua kila kitu, wala hawana haja ya kujifunza zaidi. Hii ni tabia mbaya ambayo huzuia kabisa maendeleo" (Tujisahihishe, 1962, JK. Nyerere)

Sababu za mtu kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa kiongozi zipo nyingi nje ya kuangalia uwezo wake wa kiakili, kwahiyo ni wazi kwamba ukisha kuwa kiongozi haimaanishi unajua zaidi kuliko wengine, bali hatuwezi kuwa viongozi wote na hivyo ni muhimu kushirikiana kwa kiwango sawasawa katika kutoa maoni na mawazo ili kuleta tija kwenye nchi.

Lazima nikiri wazi kwamba uongozi unahitaji akili japo akili hizo hazitokani na madaraka. Unapokuwa na dhamana kubwa yenye uwezo wa kuteua, ambayo kila mtu anaona unaweza kumpa kazi ni muhimu kuwa makini na wapiga zomali, maana nao wanatumia akili hiyo kupata au kutimiza malengo yao.

Usipokuwa na akili unaweza kudhani kwamba wanakupenda sana, ukweli utajulikana siku umeyakosa madaraka yenyewe.

Katiba yetu inatamka wazi kwamba msingi wa madaraka unatoka kwa wananchi, hivyo iwe ni uongozi wa kitaifa au wa ofsi ni muhimu zaidi watu kupewa nafasi ya kushiriki moja kwa moja katika uongozi wao, japo nakubali kwamba si kila jambo ni la kushirikisha, hayo yanajulikana, lakini yale unayodhani ni haki yao washirikishe, wakati mwingine watakufanya uwe kiongozi bora zaidi.

Viongozi wengi mashuhuri duniani ambao wamewahi kutoa hotuba zikabaki kwenye kumbukumbu za dunia hii, ukichunguza zaidi utagundua kwamba pamoja na uwezo wao wa akili, wamezungukwa na watu wenye akili nyingi zaidi ambao wamepewa nafasi ya kutumia uwezo wao wa kiakili katika kuhakikisha mambo yanakwenda vema na mwisho wa siku sifa na utukufu unaonekana kwa kiongozi husika.

Mwalimu anayefikiri kwamba wanafunzi ni wajinga hawajui chochote anaweza kuwa mjinga zaidi kuliko wanafunzi wenyewe, kwasababu mwanzo wa elimu ni kutambua kuwa hatujui kitu hivyo kila wakati tunahitaji kujifunza kwa yeyote au kwa chochote. Kama ambavyo uelewa unatofautiana ndivyo ilivyo kwa ujinga pia hutofautiana na kwamba mjinga wa jambo hili hawezi kuwa mjinga wa jambo lile.

Mwisho ni rai yangu kwa viongozi wote, kumbukeni kwamba madaraka hayawapi uhalali wa kufahamu kila kitu kwani kutokuwa kiongozi hakumaanishi ni kukosa akili, usipokuwa makini unaweza kujikuta unawaongoza viongozi wako. Kiongozi anaweza kuwa yeyote, ndiyo maana leo anatumbuliwa huyu anateuliwa yule.

Wengine walikuwa chini yako leo ni mabosi zako. Hivyo ukiyapata madaraka lazima kuyatumia vizuri, maana walioko chini yako kesho watakuwa viongozi wako kisha utashindwa kuwatazama usoni kwasababu mwanzo ulifikiri wewe pekee ndiye mwenye akili, kumbe jamaa wanakuzumu tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mishono ya 'Mwanameka' 'Zembwela' ilivyotikisa



Na Adam Fungamwango

**Mitindo hiyo ilisababisha mafundi cherehani kuwa na kazi kubwa ya kuwashonea wanawake wa enzi hizo. Kama fundi cherehani hakuweza kushona magauni ya mitindo hiyo, basi hakuweza kupata wateja wengi kwenye ofisi yake au sehemu anayofanyia kazi.**

KWA sasa tunaona kinadada wakiwa wamependeza na nguo zao za mitindo mbalimbali wanapopita barabarani.

Wasichana na kinamama wa sasa mara nyingi nguo zao hununua moja kwa moja madukani, ni tofauti na wale za zamani ambao walikuwa wakinunua vitambaa na kwenda kushona kwa mafundi cherehani.

Ni kwa sababu siku hizi nguo zimekuwa nyingi za mitindo mbalimbali na zinapatikana kwa urahisi tofauti na zamani.

Wakati kinadada wa sasa wakijipamba na nguo za mitindo mbalimbali, zamani pia kulikuwa na nguo nzuri za mitindo mbalimbali ambayo wanawake walivaa na kupendeza.

Baadhi ya mitindo ya magauni ilikuwa ni 'mwanameka', 'zembwela', 'nguva' na mingine mingi.

Mitindo hiyo ilisababisha mafundi cherehani kuwa na kazi kubwa ya kuwashonea wanawake wa enzi hizo.

Kama fundi cherehani hakuweza kushona magauni ya mitindo hiyo, basi hakuweza kupata wateja wengi kwenye ofisi yake au sehemu anayofanyia kazi.

Fundi cherehani yeyote ilibidi ajifunze kushona magauni ya mitindo hiyo ili apate wateja.

Tukianza na gauni la mtindo wa zembwela ni kwamba kinadada, mafundi na wanamitindo wa wakati huo, walifanya ubunifu na kuibuka na gauni wakaliita jina hilo.

Ni jina lililotokana na mtindo wa muziki wa bendi ya Maquiz Original chini ya Nguza Viking maarufu kwa sasa kama 'Babu Seya'.

Ni mtindo uliovuma sana wakati huo nchini Tanzania katikati ya miaka ya 1980 hadi 1990, kiasi cha wanamitindo wa mavazi kuipa gauni jina hilo.

Mtindo wa Zembwela ulikuja baada ya Maquiz kuachana na mtindo wao wa zamani wa 'Ogelea Piga Mbizi'.

Upinzani mkali kati ya bendi hiyo na Orchestra Safari Sound iliyokuwa na mtindo wa 'Dukuduku' chini ya Fredie Ndala Kasheba, ulisababisha Maquiz kuachana na 'Ogelea Piga Mbizi' na kuja na mtindo mpya wa 'Zembwela'.

Ni kwa sababu wakati Maquiz wanasema 'Ogelea Piga Mbizi', OSS wao walikuja na mtindo wa 'Chunusi' kitu ambacho kilionekana kama ni kijembe.

Walikuwa na maana kuwa wote wanaogelea kwenye bahari basi wanachukuliwa na chunusi.

Kibiashara iliwaharibia Maquiz na kuja na mtindo mwingine wa 'Zembwela' ambao uliwaibua tena Maquiz na kuja juu kimuziki.

Mtindo wa Zembwela ambao maana yake kizaramo ni 'zurura' ukawa maarufu sana mpaka wabunifu wakategeneza gauni na kuliita kwa jina hilo. Mwanzoni mwa miaka ya 1980, pia kulikuwa na mtindo mwingine wa gauni uitwao 'Mwanameka'.

Mtindo huu wa gauni ulitokana na wimbo wa bendi ya Dar International, uliotungwa na Marijani Rajab, uitwao 'Mwanameka'.

Wimbo huo ukawa maarufu sana kiasi cha kubuniwa gauni na likapewa jina la wimbo huo.

Magauni ya mtindo wa Zembwela na Mwanameka yakawa maarufu sana kwa kinadada kiasi cha dada yeyote wa kisasa wa wakati ule ni lazima awe na magauni hayo.

Ukiachana na mitindo hiyo ya magauni kwa kinadada, tunakuwa na kinakaka.

Wao walipenda kuvaa mashati ya 'Juliana' au ya ndege. Hata hivyo, si wote waliokuwa na uwezo wa kumudu kununua au kuwa na mashati hayo.

Ndiyo mashati yaliyokuwa ghali sana wakati huo na yalivaliwa na watoto wa mjini, na si kila kijana alikuwa nayo.

Mashati hayo yaliingia nchini yakitokea Burundi. Yaliingizwa na wafanyabiashara waliokuwa wakienda nchini huko kuchukua bidhaa kama sabuni, nguo na vitu.

Ikumbukwe kuwa wakati huo nchini Tanzania kulikuwa na mdororo wa uchumi kutokana na athari za vita ya Kagera.

'Mabitozi' wa wakati huo walivaa mashati hayo ambayo mengi yalikuwa na rangi ya bluu na nyeusi, huku kukiwa na ndege aliyechorwa pembeni ya kifua.

Upande wa viatu kulikuwa na raba mtoni, chachacha, na aina fulani ya viatu vya pastiki ambavyo vilikuwa vinaunguza sana ikifika saa sita mchana, maarufu wakati huo kama 'saa sita utanikoma'.

Hivi vilivaliwa zaidi na wanafunzi. Pia kulikuwa na raba maarufu za DH, bila kusahau katambuga.

Katambuga ni aina fulani ya kandambili ambazo zilitengenezwa kwa kutumia matairi ya gari yaliyochongwa.

Miaka ya 1980, baada ya mdororo wa uchumi kutokana na Vita ya Kagera, lakini pia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kandambili hizi kama za siku hizi, ziliadimika nchini na Wabongo walilazimika kuvaa katambuga hadi katikati ya miaka ya 1990, hali ilipoanza kuwa nzuri.

HADITHI

## HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Alivaa kijora na viatu vya kawaida tu. Nywele zake alisuka mabutu.

Alishindwa kusema chochote. Donald naye alishindwa kumkaribisha.

"Karibu." Sadiki alisaidia.

Tausi alibaki amesimama. Hakujua akae au aendelee kusimama.

"Kaa hapo." Sadiki aliendelea kusimamia shoo ya watu ambao walikuwa hawaongei.

"Ka'Sadiki yaani umenikurupusha huko, sijaoga, sijabadilisha nguo, nilivyokuwa ndiyo hivi hivi jamani. Si ungeniambia ili angalau nikaoge tu jamani?"

"Siyo mimi Tausi. Aliyekwita ni huyu hapa. Mi mjumbe tu. Na siku zote Mjumbe hauawi."

"Samahani Tausi. Mimi ndiyo niliyekwita." Donald alidakia.

"Na niliyemwita ni Tausi. Tausi kama yeye bila kujali yukoje na amevaa nini. Hata ungekuja umevaa gunia wala nisingejali." Alisema na kusababisha vicheko kutoka kwa wenzake.

"Usijali, kuna siku nitakwambia mapema kuwa nakuja, na kukuachia masaa ya kujipamba kama malkia." Baada ya kumaliza maneno hayo vicheko vilizidi.

"Ni hivi Tausi, mimi nimekuja kukuangalia tu mgonjwa wangu. Unaendeleaje?"

"Mimi nimeshapona. Nashukuru sana kwa msaada wako kusema kweli. Mimi sikutegemea hili. Nakushuru sana."

"Tuachane na hayo. Pesa zako za mchezo umeshalipwa?"


Ndipo Tausi alipokumbuka kuwa alishawahi kumwambia kuwa anadai pesa zake na mchezo ambazo ndizo zilikuwa amlipe dada aliyekuwa anapigana naye, Tatu.

"Nusu nimelipwa, zingine bado."

"Sasa kwa nini huwa mnacheza michezo ambayo hamlipani?"

"Kaka yangu we acha tu. Unajua sisi wanawake walimuona mwenzao mnyonge ndiyo wanafanya hivyo. Wale wakorofi thubutu. Sisi ambao ukorofi wetu ni wa midomo tu tunadhulumiwa."

"Kifupi Tausi nahitaji au napenda kama utakuwa na nafasi, Jumapili ijayo kama hutojali nije kukuchukua pamoja na Sadiki. Nataka twende sehemu moja tulivu kusherehekea mimi na rafiki yangu Sadiki kukutana baada ya miaka mingi. Nimesoma naye huyu. Na nimekuchagua wewe kwa sababu ni kama nimeshaanza kukuzoea, tangu siku ile pale kwenye ugomvi."




**"Hapana, mimi pia ni mwanamke, lazima niwe na wivu. Maana hata mama hapa nilimuuliza, akaniambia hujamuaga na ulirudi usiku mkubwa sana wakati si kawaida yako."**

Tausi hakupinga. Alijiona mwenye bahati kubwa. Akimuangalia kijana yule alionekana kama ni mtu makarimu, mcheshi na mwenye uwezo.

Hata alipoondoa Tausi hakulala usiku. Alimuwaza na kumuota pia. Yeye ni mtoto wa kike. Aliziona dalili zote za upendo kwake ndani ya kijana yule ambazo hajazidhihirisha wazi.

****************************

Ndipo Donald alipogundua kuwa moyo wake umempenda Tausi na si kingine. Kile ambacho kilichokuwa kikimsumbua moyoni na yeye mwenyewe kukikataa kuwa siyo hicho, kimeshindikana.

Ni kwamba ameshindwa kuudhibiti moyo wake.

"Hivi kinachopenda ni mtu mwenyewe au moyo?" Alijiuliza.

Kwa yeye mwenyewe alijiona hadhi yake ni kubwa mno kumpenda mwanamke kama Tausi.

Mwanamke wa uswahilini, asiye na elimu. Ambaye kazi yake ni kushinda vibarazani na wanawake wenzake kusengenyana, kusutana na kwenda kugombana na wenzao.

Kutwa kuangalia nani kala nini, nani kavaa nini. Kubwa kuliko yote ni ile ya kupenda vigoma vya Uruguay na vigodoro.

Angeweza kujidhibiti na hilo, lakini moyo wake ulionekana kuangukia kwa msichana huyo. Hawezi kushindana na moyo wake.

"Nampenda sana Tausi." Alijiambia mwenyewe.

Tatizo lilikuwa kwa wazazi wake. Alijua angepata upinzani mkali kutoka kwa wazazi wake.

Mbali na kwamba hawakupenda mwanamke ambaye anatoka uswazi, lakini pia tayari walikuwa wameshampatia mwanamke, Doris.

Alijiuliza atasimama vipi mbele yao kuwaambia kuwa hamtaki tena Doris na chaguo lake lipo kwa Tausi?

Ilikuwa ni siku tatu tu tangu walipokuwa kwenye hoteli moja kule Kigamboni ambayo aliiandaa mwenyewe. Walikuwa watu wanne. Rafiki yake Sadiki na mpenzi wake. Yeye na Tausi. Huko ndipo walipojuana zaidi na msichana huyo. Na ndiyo siku ambayo alimuona Tausi akiwa amependeza mno kuliko siku zote.

Ingawa alianza kumpenda siku ile ya kwanza alipoamua ugomvi na mwenzake, lakini kwenye pati hiyo Tausi alijikwatua kisawasawa.

Mara alisikia mlango ukigongwa. "Fungua." Alijibu.

Doris aliingia ndani. Kabla hajamfikia pale alipo, Donald alipata harufu ya marashi.

"Juzi kutwa nzima hukuwepo hapa nyumbani na hata simu yako ilikuwa imezimwa, ulikuwa wapi?" Doris alianzisha mjadala mara tu baada ya kuingia.

"Ina maana hiyo ndiyo salamu?"

Ndipo Doris alipogundua kuwa alikosa. Tatizo alikuwa na haraka sana. Pia hakutegemea kama jibu lake litakuwa hilo.

"Samahani, nilikuwa nauliza tu."

"Unasikia Doris." Alisema Donald akiinuka kutoka kitandani alipokuwa amejilaza na kukaa.

"Mimi na wewe hatujafika muda wa kuanza kuulizana ulikuwa wapi na ulikuwa unafanya nini, unasikia." Donald alisema kwa sauti ya ukali kidogo.

"Wewe umeletwa hapa na mama na baba uwe mchumba wangu. Hata uchumba wenyewe bado umeanza kunichungachunga, nikikuoa si ndiyo utanifunga kamba kabisa?"

"Hapana, mimi pia ni mwanamke, lazima niwe na wivu. Maana hata mama hapa nilimuuliza, akaniambia hujamuaga na ulirudi usiku mkubwa sana wakati si kawaida yako."

Donald alimuangalia Doris kwa makini na kama alikuwa anataka kusema kitu, lakini alisita.

Doris mwenyewe alishtuka na kujua kuna kitu kinamtatiza. Au anataka kuongea.

"Sikiliza Doris. Leo nataka nikwambie kitu. Nataka kukwambia ukweli wote."

"Kuwa hunitaki?" Doris alidakia.

"Hapana, siyo kwamba sikutaki. Na usiwe na haraka hivyo." Donald alinyanyua chupa ya maji na kunywa mafunda kadhaa, akaiweka kwenye meza ndogo pembeni mwa kitanda.

"Ni kwamba wewe ni mwanamke mzuri, mrembo na una sifa zote za kuitwa hivyo. Msomi na umetoka kwenye familia ya kitajiri. Lakini moyo wangu haujaridhika na hautoridhika kuwa na wewe." Alisema na kushusha pumzi. Ni kama vile alikuwa amemaliza kazi ya muda mrefu. Kwa muda sasa alikuwa anataka kumwambia hivyo, lakini aliogopa.

Kwanza kabisa hakuwa na uhakika wa kumpata Tausi. Alikuwa hajakaa na kuongea na Tausi na kumfahamu vema.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# FEZA KUWA KARIBU NA D'BAJI

MSHIRIKI wa zamani wa shindano la Big Brother Africa (BBA), Feza Kessy, ameweka wino katika dili la kusimamiwa na mwanamuziki wa Nigeria D'baji.

Feza amejiunga katika familia ya mwanamuziki huyo kupitia lebo yake ya 'DB Records' iliyopo Lagos.

Mtanzania huyo amekaribishwa kupitia ukurasa rasmi wa instagram wa Bangalee, hivyo anakuwa msanii wa kwanza wa kike.

## AY aikubali 'Ona' kwa sana

MWANAMUZIKI mkongwe nchini, AY ameitabiria mema Album mpya ya mtengezaji wa muziki, Marco Chali, akisema ni moja ya kazi itakayoishi muda mrefu.

Albam hiyo inayoitwa 'ONA' itazinduliwa rasmi Mei 28 mwaka huu.

"ONA Album mpya ya Marco Chali inakuja mwezi huu, hii ni kati ya Album classic kabisa inayotabiri kuwa nyimbo zake zitaishi kwa kipindi kirefu sana kutokana na jumbe tofauti zilizoimbwa humo, stay tuned" amesema AY



## Jitu Baya aisifia 'Nyama' mpya

MWANAMUZIKI anayekuja kwa kasi katika muziki wa Hiphop, Jitu Baya, ameangusha kazi yake nyingine mpya inayoitwa 'Nyama' kama zawadi ya Eid El fitr.

Akizungumza na Gazeti hili, Jitu Baya, amesema wimbo wake huo utakuwa zawadi tosha kwa mashabiki wake ambao wanamuunga mkono kwa kila hatua anayopiga.

"Natumaini wimbo wangu 'Nyama' utakuwa zawadi tosha kwa mashabiki wangu, nafurahi sana kuwaona wananiunga mkono na kufuatilia kazi zangu kila ninapozitambulisha," amesema.

Ngoma yake hiyo tayari inapatikana katika akaunti yake ya You Tube na umeanza kuchezwa katika vituo mbalimbali vya redio hapa nchini.



# Bayern yakataa kumuuza Lewandowski

**MUNICH,** Ujerumani

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, amejibu juu ya uvumi unaoendelea wa kuondoka kwa Robert Lewandowski, na kuweka wazi kuwa kitu kama hicho hakiwezi kutokea kwa sasa.

Iliripotiwa kuwa mabingwa hao wa Ujerumani wanaweza kuwa tayari kuachana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kama watafanikiwa kumsajili Erling Haaland kutoka Borussia Dortmund.

Lewandowski kwa sasa anakaribia kuvunja rekodi ya kufunga mabao 40 kwa msimu mmoja huu wa 2020-21 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, na Rummenigge amesema hakuna nafasi ya kuondoka hapo Allianz Arena hivi karibuni.

Bayern hawana haja ya kuzingatia uvumi unaoendelea kwa Lewandowski kwani uwapo wa mchezaji huyo ambaye ndiye mfungaji bora umefungwa kwa mkataba hadi mwaka 2023.

Haonyeshi ishara ya kupungua kiwango, baada ya kufunga mabao mengine 46 kwenye mashindano yote msimu huu, na amezungumza juu ya hamu ya kucheza kwa angalau miaka mingine mitano.

"Hakika yupo hapa. Ni nani anayeuza mchezaji anayefunga mabao 60 kwa mwaka?" Alihoji Rummenigge akiiambia Sport1.

"Ni matumaini yangu atakaa kwa muda mrefu hapa Bayern Munich."






# TOTTENHAM SASA KUMBAKIZA BALE

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur ina mpango wa kumwongezea muda wa mkopo, Gareth Bale ambaye yupo hapo akitokea Real Madrid.

Kwa mujibu wa Dail Mail, Mwenyekiti wa timu hiyo, Daniel Levy anafanya jitihada kuhakikisha kwamba, Bale anabakia kikosini hapo kwa msimu wa 2021/22.

Raia huyo wa Wales mkataba wake na Real Madrid unatarajiwa kufika tamati Juni 20, mwakani.

Bale amekuwa akiweka wazi kwamba, anahitaji kurejea katika timu yake ya Real Madrid ili kupata changamoto tena chini ya Kocha Mkuu, Zinedine Zidane kwa kuwa ameshapata uzoefu.

Lengo la nyota huyo ni kwenda kumalizia mkataba wake katika timu yake tofauti na hapo alipo kwa sasa.

Hata hivyo, mahusiano ya Bale na Zidane si mazuri na ndio yaliyosababisha kupelekwa kwa mkopo kule Spurs baada ya kukosa nafasi katika dimba la Santiago Barnabeu.

Kwa mujibu wa ripoti, Levy sasa anaona nyota huyo anaweza kuendelea kucheza hapo kwa sababu amekuwa na wakati mzuri.

# *Fernandes: Tumejifunza kutokana na makosa*

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester United, Bruno Fernandes, amesema kila mchezaji alipoteza furaha baada ya kichapo mbele ya Liverpool katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Ikiwa Uwanja wa Old Trafford ubao ulisoma Man United 2-4 Liverpool na kuwafanya waache pointi tatu zikielekea kwa wapinzani wao.

Fernandes amesema walijipanga kupata ushindi ila mambo yakawa magumu kwao.

"Ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo kila mchezaji hakuwa na furaha na hatujafurahi kweli kufungwa," alisema Fernandes akinukuliwa na BT Sport.

"Wametumia makosa yetu na tumeona makosa yetu tutajifunza kupitia makosa.

"Msimu huu mambo yamekuwa magumu kidogo kwetu, lakini naamini tutakuwa na wakati mzuri zaidi kwa msimu unaokuja.

Kila mmoja amejipanga kuhakikisha kwamba, makosa ya safari hii hayajitokezi tena kwa msimu unaokuja."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND MBADALA WA MESSI BARCELONA

●●● Ni wakati nguli huyo wa Argentina akihusishwa na miamba ya Ligi Kuu England, huku...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA ina nia kubwa ya kumsajili Erling Haaland hapo Camp Nou na kwamba, ipo tayari kumuachia nahodha wake, Lionel Messi kuondoka, kwa mujibu wa The Sun.

Miamba hao wa Catalunya wameripotiwa kuwa kama wakifanikiwa kumsajili Haaland kutoka kule Borussia Dortmund hawatakuwa na tatizo la kuachana na Messi ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Messi ametumia karibia kipindi chake chote cha uchezaji hapo Barcelona na bado hajafikia mwafaka wa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo.

**Kabla ya kuanza kwa msimu huu, Messi aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka Barca kabla ya kubadili maamuzi na kuamua kubaki.**

Na sasa ni wazi kwamba, bado kuna kizungumkuti cha nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kama atakubali kusaini mkataba mpya.

Hivyo, Barcelona wanaona kwamba, Haaland raia wa Norway mwenye umri wa miaka 20, anaweza kuwa mbadala wa kudumu wa Messi.

Hali ya kiuchumi kwa Barca sasa ni mbaya na hivyo kwa vyovyote itakuwa katika wakati mgumu kuweza kumlipa mshahara mkubwa mchezaji kama Messi.

Kwa mujibu wa ripoti, Messi atajikuta mshahara wake ukikatwa nusu kama ataamua kubakia hapo.

Messi amekuwa akihusishwa na miamba ya Ligi Kuu England, Manchester City na Paris Saint-Germain.

Kwa upande wa Haaland, amekuwa akiwaniwa na klabu kadhaa ikiwamo Man City, Manchester United, Real Madrid, Chelsea, PSG, Liverpool, Bayern Munich na Juventus.

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUTUA MAN UTD

VYANZO vya karibu kutoka Borussia Dortmund vimeeleza kwamba, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21, anajiamini zaidi kuwa uhamisho wake wa kwenda Manchester United utakamilika kipindi hiki cha majira ya joto. Miamba hao wa Ligi Kuu England wanatarajia kutoa ofa ya pauni milioni 65 hadi 75 ili kupata saini ya nyota huyo wa England. ***(Eurosport)***

### LINGARD AGEUZWA CHAMBO

MANCHESTER United inaweza kumtumia mshambuliaji wa wake, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, kama chambo ya kumpata Jadon Sancho. ***(Sun)***

### PSG YAMUWANIA SALAH

KLABU ya Paris Saint-Germain inafikiria kumsajili straika wa Liverpool, Mhohamed Salah mwenye miaka 28, kama mbadala wa Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22. ***(ESPN)***

### HODSON KUONDOKA PALACE

ROY Hodgson anatarajia kuondoka Crystal Palace wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Times)***

### ARSENAL KUMUACHIA CEBALLOS

ARSENAL haina mpango wa kuongeza muda wa mkopo kwa kiungo wa Real Madrid, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 24. ***(Independent)***

### UNITED YAMTAKA VARANE

MANCHESTER United ipo kwenye mazungumzo na mlinzi wa Real Madrid, Raphael Varane, mwenye umri wa miaka 28. ***(Manchester Evening News)***

### KONATE ANA KIPENGELE

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RB Leipzig, Oliver Mintzlaff, amethibitisha kwamba, mlinzi wa Ufaransa, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21, ambaye anawaniwa na Liverpool ana kipengele cha fedha ya kuondoka katika mkataba wake. Katika kipengele hicho, nyota huyo anatakiwa kuuzwa kwa pauni milioni 34. ***(Liverpool Echo)***

### MENDES AWANIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inataka kumsajili mlinzi wa pembeni wa Sporting Lisbon, Nuno Mendes mwenye umri wa miaka 18, ambaye thamani yake ni pauni milioni 52. ***(Mail)***

### TUCHEL APEWA CHAGUO

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amepewa chaguo la kumsajili straika wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, au mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye miaka 28. ***(Express)***

### PULISIC AKANA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, amekanusha uvumi kwamba anaweza kuondoka hapo Stamford Bridge kipindi hiki cha cha majira ya joto. ***(ESPN)***

## Kakolanya, Gadiel kuanguka miwili Simba

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba unaendelea na mchakato wa kuongeza mikataba majembe yao akiwamo beki, Gadiel Michael na kipa Beno Kakolanya, kwa ajili ya kuendelea kutumikia timu hiyo kwa msimu mpya.

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili jijini jana kutoka ndani ya klabu hiyo, zinaeleza uongozi tayari umefanya mazungumzo na nyota hao na muda wowote wataangusha saini ya mkataba wa miaka miwili kila mmoja.

Alisema wawili hao walitakiwa kuongeza mkataba mapema kabla ya mechi dhidi ya Yanga, lakini ilishindikana kwa sababu aliyekuwa na jukumu hilo alisafiri kwenda nje na sasa watakaporudi kutoka Afrika Kusini ambapo jana usiku timu yao ilicheza dhidi ya Kaizer Chiefs kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, watamwaga wino.

"Kwa hiyo muda wowote Kakolanya na Gadiel wataongeza mikataba ya kuendelea kuitumikia Simba kwa sababu ni mapendekezo ya Kocha Mkuu, Didier Gomes, aliyeorodhesha majina ya wachezaji anaohitaji kuwapo katika mipango yake," alisema kigogo huyo.

Alisema nyota hao wawili wataungana na wengine akiwamo Mohammed Hussein 'Tshabalala', John Bocco, Shomari Kapombe, Kennedy Juma na Erasto Nyoni, ambao wameshamwaga wino.

"Wachezaji wote wanaongezewa mikataba wako kwenye mipango ya Gomes na kuwataka baadhi ya majembe yao kuendelea nao kwa msimu ujao," alisema kigogo huyo.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema uongozi uko makini katika kutimiza mapendekezo na mahitaji ya kocha Gomes likiwamo suala la usajili wa wachezaji watakawaona wanaweza kuisaidia klabu hiyo kufikia malengo.

"Tunahakikisha tunatimiza mahitaji yote ya kocha Gomes, hivyo tulianza na baadhi ya wachezaji kuwaongeza mikataba na zoezi litaendelea kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi," alisema mtendaji huyo.

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS BINGWA LIGI KUU KUJULIKANA LEO

**Na Saada Akida**

KITENDAWILI cha nani bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, kitaamuliwa leo wakati vigogo wa soka hilo nchini, Simba Queens na Yanga Princess watakaposhuka dimbani katika viwanja tofauti kuhitimisha mbio za kinyang'anyiro hicho msimu huu wa 2020/21.

Ligi hiyo inahitimishwa leo kwa michezo mitano, Simba Queens ambayo ipo kileleni ikiwa na pointi 51, itakuwa ugenini katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma dhidi ya Baobab Queens na Yanga Princess waliopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo wakiwa na alama 50, watakuwa wenyeji wa Alliance Girls ya Mwanza katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Endapo Simba Queens itashinda leo, itafanikiwa kutetea ubingwa huo kwa mara ya pili mfululizo, lakini pia ikipoteza na Yanga Princess kushinda, basi watani zao hao watalibeba taji hilo kwa mara ya kwanza.

**Na ushindi wowote kwa Yanga Princess leo huku Simba Queens ikitipoteza ama kutoka sare, maana yake ni kwamba miamba hiyo ya Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam itakuwa mabingwa.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema malengo yao ni kutetea ubingwa na watahakikisha wanapambana kutafuta pointi tatu dhidi ya Baobab Queens.

"Lengo letu lilikuwa ni kuwa mabingwa mapema, ila Mungu alikuwa na mipango yake na imebidi tusubiri hadi mechi ya mwisho, Naamini tunaenda kutafuta ushindi na tunakwenda kuwa mabingwa kwa mara ya pili mfululizo," alisema Mgosi.

Kwa upande wa Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema wanachokifanya ni kwenda kuendelea kutafuta matokeo mazuri katika mechi yao ya mwisho dhidi ya Alliance Girls.

"Tunachokifanya kwa sasa ni kuwaombea mabaya Simba, hakuna kitu kingine kwa sababu najua sisi tutawafunga Alliance, dua zetu zote mbaya



Bondia Hassan Mwakinyo, anayetarajia kupanda ulingoni jijini Dar es Salaam Mei 28, mwaka huu, kuwania ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa super welter, dhidi ya Mzimbabwe Brendon Denes. **PICHA: MAKTABA**

# *Mabondia nchi tano ndani ya 'Rhumble in Dar 2'*

**Na Mwandishi wetu**

MABONDIA kutoka nchi tano za kigeni watapanda ulingoni Mei 28, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door Arena uliopo Oyesterbay, Dar es Salaam katika pambano lililopewa jina la 'Rhumble in Dar 2'.

Mabondia hao na nchi zao kwenye mabano ni Brendon Denes (Zimbabwe), Sibusiso Zingange (South Africa) Olanrewaju Durodora (Nigeria) na Chris Thompson ambaye pia anatoka Afrika Kusini.

Kwenye orodha hiyo pia wapo Ardi Ndembo anayetoka Congo Brazaville, Simon Madhanire (Zimbabwe) na mabondia wawili kutoka Bulgaria, Pench Tsvetkov na bondia nyota wa kike, Joana Nwamerue.

Wakati Denes atazichapa na bondia nyota wa Tanzania Hassan Mwakinyo kuwania ubingwa wa Afrika (ABU) wa uzito wa super welter, Zingange atashuka ulingoni kuzichapa na bondia Ibrahim Class katika pambano la uzito wa light.

Bondia Durodora atapambana na nyota mwingine wa Tanzania, Shaban Jongo katika uzito wa Cruiser wakati bondia mkali wa uzito wa juu wa Congo Brazzavile, Ndembo atazichapa na Simon Madhanire wa Zimbabwe wa uzito wa juu (heavy).

Pia kutakuwa na mapambano yanayowahusisha mabondia Thompson (Afrika Kusini), Joana Nwamerue (Bulgaria) na Pencho Tsvetkov pia wa Bulgaria katika usiku huo ambao umedhaminiwa na Benki ya Wadhamini ambao ni Benki ya KCB, Bodi ya Utalii, DStv, Onomo Hotel, M-Bet ma Plus Networks Limited.

Mapambano hayo yameandaliwa na Kampuni ya Jackson Group Sports kwa kushirikiana na Global Boxing Stars na Epic Sports and Entertainment.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, amesema mabondia wote wapo katika mazoezi makali kuelekea siku hiyo.

Twissa amesema mabondia kutoka nje ya nchi wanatarajiwa kuwasili nchini kuanzia wiki ijayo tayari kwa usiku huo.

"Maandalizi yanakwenda vizuri, tiketi zimeanza kuuzwa kupitia 'app' za nilipe na 'ontapp' ambapo siti za kawaida ni Sh. 50,000 na VIP Sh. 200,000," alisema Twissa.

# Michezo

Jumapili Mei 16, 2021

Nipashe




Haaland mbadala wa Messi Barca UKURASA 22

HAPO MWISHO...



Winga wa Simba, Luis Miquissone, akimtoka beki wa Kaizer Chiefs kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa FNB na Simba kuangukia pua kwa mabao 4-0. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAKUTANA NA KINYOZI MBABE SAUZI

## ●●● Yauchezea mpira ikimiliki 65% kwa 35% lakini yanyolewa nne, sasa mlima mrefu nusu fainali CAF...

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara ya kwanza msimu huu wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba imekutana na 'kinyozi mbabe' ikiwa Afrika Kusini baada ya kukubali kunyolewa mabao 4-0 katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa FNB nchini humo jana.

**Mabao matatu ya vichwa na moja la mguu wa kulia, yaliyotokana na uzembe wa mabeki wa Simba, yameisababishia timu hiyo kujiweka kwenye mazingira magumu ya kusonga mbele hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku yakiifaidisha Kazer Chiefs.**

Wachezaji wa Simba ambao wengi walionekana kutokuwa kwenye kiwango chao cha kawaida, wameiweka kwenye mazingira magumu timu hiyo kusonga mbele kwenye mechi ya marudiano inayotarajiwa kuchezwa Jumamosi ijayo Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Ili isonge mbele Simba ambayo ilimiliki mpira kwa asilimia 65 dhidi ya 35 huku ikipiga jumla ya pasi 579 kwa 303, sasa inatakiwa ishinde mabao 5-0 katika mechi ya marudiano.

Kwenye mechi hiyo, Simba ilianza kunusurika kufungwa dakika ya nne tu, baada ya Lebogang Manyama kumlamba chenga kipa Aishi Manula kutokana na makosa ya walinzi wa timu hiyo, lakini aliupiga mpira nje. Makosa mengine ya walinzi wa Simba yaliifanya Kaizer Chiefs kuandika bao la kwanza dakika moja baada kupitia kwa beki namba nne wa timu hiyo, Erick Mathoho aliporuka juu na kupiga kichwa mpira wa kona uliopigwa na Njabulo Blom.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuichanganya Simba, huku wachezaji wa timu hiyo wakipoteza mipira mingi na dakika ya 10, Chriss Mugalu nusura aisawazishie Simba, lakini beki Siyabonga Ngezana aliucheza na kumfanya apige hewa.

Bao la pili la Kaizer Chiefs lilifungwa dakika ya 34 na straika hatari wa timu hiyo raia wa Serbia, Samir Nurkovic kwa kichwa, baada ya krosi ilipopigwa upande wa kulia, huku mabeki wa Simba wakimtazama.

Manula aliiokoa Simba kufungwa bao dakika ya 37 alipookoa kwa ustadi mpira wa kichwa uliopigwa na Ngazana. Dakika mbili baadaye Clatous Chama aliikosesha Simba bao baada ya kupata pasi kutoka kwa Luis Miquissone, lakini mpira wake alioudokoa ulimgonga kipa Bruce Bvuma na mpira ukatoka nje.

Kipindi cha pili kiliendelea kuwa vile vile kwa wachezaji wa Simba kupoteza nafasi nyingi na mabeki kukosa umakini. Alikuwa tena Mserbia Nurkovic aliyeipatia Kaizer Chiefs bao la tatu kufuatia makosa ya Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambaye aliupiga kichwa mpira kumrudishia kipa Aishi Manula, lakini ilimkuta straika huyo hatari ambaye aliruka na kujipindua, akiupiga kwa mguu wa kulia, mpira ukakwama wavuni.

Alikuwa ni raia wa Colombia, Leonardo Castro aliyeondoa matumaini ya Simba kwenye mechi hiyo alipofunga bao la nne kwa kichwa, akiunganisha mpira wa krosi ya mbali kutoka kwa Manyama, iliyowapita vichwani mabeki wa Simba.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes aliwatoa Jonas Mkude, Rally Bwalya na Miquissone, nafasi zao zikichukuliwa na Hassan Dilunga, Meddie Kagere na John Bocco, lakini haikuwa siku nzuri kwa Wekundu wa Msimbazi hao.

# Yanga ubingwa bado ni mgumu

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa kihistoria, Yanga, wamejiweka kwenye mazingira magumu ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya kwanza baada ya misimu mitatu kutokana na kuambulia suhulu dhidi ya Namungo FC.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, timu hizo ziligawana vipindi, Yanga ikitawala kipindi cha kwanza na Namungo FC ikiamka kipindi cha pili.

Pamoja na kusalia nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, suluhu hiyo inaipa zaidi nafasi Simba kama ikifanya vizuri kwenye mechi zake zijazo. Yanga imefikisha pointi 58 huku ikiwa imecheza mechi 28, tatu mbele ya Simba iliyopo kileleni na pointi zake 61.

Namungo FC ingeweza kujipatia bao mapema tu dakika ya nane, kama mchezaji wake Hashim Manyanya asingekuwa na papara baada ya kupokea pasi safi kutoka kwa Reliants Lusajo na kumlamba chenga Adeyum Selemani, akabaki peke yake na kipa Metacha Mnata, lakini alipiga shuti dhaifu kwa mguu wa kushoto ulioitoka sentimeta chache langoni mwa Yanga.

Yanga ilifanya shambulio la nguvu langoni mwa Namungo FC kwenye dakika ya 20, wakati Mrundi Saido Ntibazonkiza alipowapokonya mpira wachezaji wa timu pinzani, akampasia Michael Sarpong aliyemrudishia tena mchezaji huyo na kukimbia kwa umbali mrefu akiwa peke yake, lakini mbio zake hazikufua dafu kwa wachezaji Steven Duah na Frank Magigi ambao walimfikia na kuokoa kabla ya kumfikia kipa Jonathan Nahimana.

Almanusura Yanga wapate bao dakika ya 24, lakini shuti la Zawadi Mauya aliyekuwa ameuganisha mpira wa kona kutoka kwa Ntibazonkiza, ulimgonga mchezaji mmoja wa Namungo FC kwa bahati mbaya na kutoka nje.

Kipa Nahimana alilazimika kufanya kazi ya ziada dakika za kwanza kipindi cha pili, kutoka kwa Yacouba Sogne pamoja na Ntibazonkiza, huku Steve Nzigamasabo akikosa bao dakika ya 79 alipopiga shuti lililopanguliwa na kipa Metacha.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


%%%%%